


MTUME WANGU KIPENZI MFANO BORA WA KUIGWA

Nehir Aydın Gökduman

Kwa watoto wa miaka 7 na kuendelea



MTUME WANGU KIPENZI MFANO BORA WA KUIGWA

Nehir Aydın Gökduman

Kwa watoto wa miaka 7 na kuendelea



© Erkam Publications - Istanbul: 1443 / 2022

**MTUME WANGU KIPENZI
MFANO BORA WA KUIGWA**
(Kwa watoto wa miaka 7 na kuendelea)

Nehir Aydin Gökduman

Jina la Kitabu halisi: En Güzel Örneğim Peygamberim

Mwandishi: Nehir Aydin Gökduman

Wafasiri: Dkt. Mussa Mohammed Hans

Mhariri: Dkt. Mussa Mohammed Hans
Hamza Daudi Msuya

Meneja wa Uchapishaji: Salih Zeki MERİÇ

Picha: Zehra ÖZDEMİR

Michoro/Usanifu: Rasim ŞAKIROĞLU

ISBN: *****

Address: Ikitelli Organize Sanayi Bölgesi Mahallesi,
Atatürk Bulvarı, Haseyad 1. Kısım No: 60/3-C
Başakşehir, İstanbul, Türkiye

Tel: (+90-212) 671-0700 pbx

Fax: (+90-212) 671-0748

E-mail: info@islamicpublishing.org

Web site: www.islamicpublishing.org

Printed by: Erkam Printhouse

Language: Swahili





MTUME WANGU KIPENZI

MFANO BORA WA KUIGWA

YALIYOMO

DIBAJI.....	5
ZAID MTUMWA MDOGO	6
UAMUZI WA ZAID.....	8
KIJANA ALIYEPENDWA NA MTUME (S.A.W).....	10
HASSAN NA HUSSEIN (R.A).....	12
NANI ALIKUWA WA KWANZA KUOMBA MAJI?	14
ANAS (R.A) MVULANA ALIYETUNZA SIRI	16
MTOTO WA KWANZA KATIKA UISLAMU	18
MVULANA ALIYERUSHA MAWE KWENYE MITI YA TENDE	20
MSICHANA MDOGO YATIMA.....	22
MTU MWAMINIFU ZAIDI	24
HUZUNI YA FATMA	26
SAHIL NA KAKA YAKE SUHAIL	28
UTUKUFU WA WITO WA ADHANA.....	30
FURAHA YA MTUMWA.....	32
MTU MASKINI	34
ZAYD MWANDISHI KIJANA	36
THALABA BIN HATIB ALIYEKUWA ANAOMBWA UTAJIRI	38
MTUME ALIPENDA SANA WATOTO	40
USHUPAVU WA ABUU MAHZURAH (R.A).....	42
ZAWADI YA MSICHANA MDOGO	44
MTUME ALIPENDA KUWA NADHIFU	46
MTU ANAYEISHI JANGWANI	48
REJESHA KIOTA CHAKE.....	50
MGENI KATIKA NYUMBA YA MTUME (S.A.W)	52
KIAPO CHA MWONGO	54

FUNZO KWA WALE WANAOKIUKA MAKUBALIANO.....	56
MTU ALIYEFANYA MOYO WA ABUDARDA KUUKUBALI UISLAMU .	58
KIJANA ALIYEMWOMBA MTUME AMWOMBEE.....	60
MGENI MASKINI.....	62
MTUME ALIISHI MAISHA YA KAWAIDA	64
USIWABAGUE WATOTO WAKO KWA SABABU YA JINSIA.....	66
MTUME ALIKUWA ANAPENDA UTANI.....	68
MTUME ALIWAHESHIMU WAKUBWA WAKE	70
WEMA WA MTUME.....	72
FURAHA YA MSICHANA MDOGO	74
EWE BILAL (R.A)! TOA ADHANA!	76
PEANENI SALAMU.....	78
KUMSAIDIA ADUI	80
USHINDI WA NAFSI	82
MTUME (S.A.W) ALIKUWA ANASIKILIZA MALALAMIKO.....	84
UVUMILIVU WA MTUME.....	86
HOTUBA YA KUAGA	88

DIBAJI

Watoto ambao kwa karne nyingi zilizopita walikuwa wakiishi na Mtume (S.A.W) walimpenda sana Mtume. Mtume (S.A.W) alikuwa akiwasalimu kwa uso wa tabasabu na wakati mwингine aliungana nao katika michezo yao na kucheza nao pamoja.

Kila mmoja alikuwa na jambo ambalo hawezi kulisahau kuhusu Mtume (S.A.W). Wapo ambao hawatasahau siku waliyokuwa wakicheza na Mtume, wengine hawawezi kusahau Mtume (S.A.W) alipokuwa akiwapapasa vichwa vyao, wengine watakumbuka namna Mtume alivyokuwa akiwatania kwa uso wa tabasamu na wengine walitunza zawadi alizowapa kama wanavyotunza siri.

Ingawa watoto hawa wanakua lakini kamwe hawawezi kumsahau Mtume (S.A.W). Mapenzi yao kwa mtume siyo mapenzi ya kwamba tu, hayaishi bali daima yanaongezeka. Walikuwa wakifurahi sana kila wanapokutana naye na walitamani kuyafikia matarajio yake. Walifurahia maisha yao kwa kiasi kikubwa wakiwa na Mtume (S.A.W).

Furaha ya marafiki wa mtume (ambao wanaitwa maswahaba) ilikuwa ni furaha ya Mtume na furaha ya Mtume ikawa ni furaha kwao pia. Macho yao yalikuwa katika mwelekeo mmoja na miyo yao ilikuwa na hisia zinazofanana.

Tunaweza kufikiria vile ambavyo maswahaba waliishi wakiwa na Mtume wetu mpPENDWA? Tunaweza kuhisi japo kidogo furaha isiyo na kifani kutoka katika miyo yao? Una maoni gani katika hili?

Huruma, upole na mapenzi ya Mtume wetu (S.A.W) vitakuwa faraja kwa miyo yetu. Sivyo?

Mwenyezi Mungu amemleta mtume awe nuru na rehema kwa ulimwengu wote. Inawezekanaje kwa mfano nuru ya Mtume isifiki miyo yetu midogo iliyojawa na mapenzi ya Mtume (S.A.W) ilihali miale ya jua inaweza kufika katika kilele cha milima mikubwa na katika kina cha bahari?

Inshallah tunaishi katika ulimwengu huu ambapo miyo yetu imejawa na mapenzi ya Mtume. kisha siku ya Qiyama tutasema:

"Tazama ewe mtume wa Mwenyezi Mungu, nimebeba mapenzi yako ya hali ya juu katika moyo wangu mkunjufu"

ZAID MTUMWA MDOGO

*M*toto mdogo aitwaye Zaid alikuwa akisononeka kwa kuwa alikuwa mbali na nyumbani tena akiwa peke yake. Mabedui walimteka kutoka katika familia yake na kumpeleka katika eneo ambalo Zaid hakulifahamu. Walitaka kumuuzza kwa matajiri ili wapate fedha.

Zaid aliishi kwa njaa, kiu na tabu kwa siku kadhaa. Alikuwa katika hali ya uchovu huku akisubiri kuuzwa katika soko la watumwa. Wauzaji wa watumwa hawakuwa na huruma kwa mtu yeyote. Walipenda fedha kuliko utu. Zaid alihofia kwamba tajiri yake si mtu mzuri. Alikuwa na hasira dhidi ya watu waliomtenganisha na familia yake.

Siku moja Zaid alipokuwa akiangalia kundi kubwa la watu kwa macho ya huzuni, mwanaume mmoja mchangamfu alimsogelea na kuanza kumuuliza.

-Unaitwa nani?

-Ninaitwa Zaid.

- Baba yako anaitwa nani?

Anaitwa Haarithah.

Alipokuwa akitaja jina la baba yake Zaid alijisikia vibaya sana. Alishikwa na huzuni kubwa kwa sababu alibaini yuko mbali na baba yake.

Baada ya hapo yule mwanaume akamuuliza:

Je, una njaa?

Zaid akatikisa kichwa chake na kubaki kimya. Hakuwa amekula kitu chochote kwa siku kadhaa. Alikuwa akitamani kupata mtu atakayemwokoa katika mazingira yale.



Yule mwanaume alimwonea huruma Zaid, na kusema:

Je, unataka kuongozana nami ukale chakula kizuri?

Zaid alimpenda mwanaume huyu mchangamfu. Nitafurahi nikiongozana nawe hata kama hakuna chakula. Zaid Alijibu.

Yule mwanaume akamlipa muuzaji ili amchukue Zaid. Kisha akamshika Zaid mkono wakaongozana na kufika nyumbani. Ilikuwa ni nyumbani kwa Khadija (r.a). Yule mwanaume mchangamfu akagonga mlango. Baada ya muda mfupi mwenyeji akatokea mlangoni. Yule mwanaume akasema:

Ewe binti wa kaka yangu! Nimekuletea msaidizi.

Khadija (r.a) akamshika Zaid kichwani kisha akamkaribisha ndani.

Zaid alihisi amani alipokuwa katika mikono ya waungwana hawa na huzuni yake ikaanza kupungua.

Baada ya muda wakakaa katika meza nzuri na kula kwa furaha.



UAMUZI WA ZAID

Miezi kadhaa ikapita. Zaid alifurahia maisha katika nyumba yake mpya. Khadija alikuwa na roho nzuri. Alimpokea Zaid kama mtoto wake na wala si kama mtumwa. Hakuwa anamkasirikia wala kumgombeza. Alikuwa mtu mzuri sana kwake.



Muda mfupi baadaye, mwanamke huyu mzuri akaolewa na Muhammad (S.A.W) mtu mwaminifu sana katika mji wa Makka. Muhammad (S.A.W) alikuwa mchangamfu na mwenye kuzungumza kwa upole sana. Aliwapenda sana watoto. Hakumpita mtoto yeoyote bila kumpapasa kichwa chake. Aliishi vizuri na Zaid kuanzia siku ya kwanza. Zaid pia alimpenda Muhammad (S.A.W) ambaye aliishi naye kwa uangalifu na ustahmilivu.

Miezi kadhaa ikapita katika hali hii. Zaid alikuwa na furaha na amani katika nyumba hii yenye baraka. Hata hivyo, kama ambavyo ingeweza kutokea kwa mzazi yeoyote aliyepotelewa na mtoto wake, wazazi wa Zaid walikuwa na huzuni sana huku wakimtafuta mtoto wao.

Baba na baba yake mkubwa
Zaid walikwenda kila mahali
nje ya Yemen kumtafuta Zaid.
Wakiwa katika harakati za



kumtafuta mtoto wao, wakafika Makka. Hatimaye wakafika katika nyumba ambapo Zaid alikuwa akiishi.

Baba yake Zaid akamwendea Mtume Muhammad (S.A.W) kisha akasema:

Nimesikia kwamba mwanangu yuko kwako. Ninataka kumchukua. Nitakupa chochote unachokitaka. Tafadhali mwache huru mwanangu.

Ingawa alikuwa na uwezo wa kukataa kumrejesha Zaid, Mtume (S.A.W) akasema:

Sasa ngoja tumwite Zaid hapa na kumuuliza anataka kusema nini? Walimwita Zaid. Mtume Muhammad (S.A.W) akamuuliza:

Zaid, unawajua watu hawa?

Zaidi aliwaangalia watu hao kwa jicho la upendo. Akasema kwa furaha:

Naam, ninawafahamu. Mmoja wao ni baba yangu na mwingine ni baba mkubwa

Baada ya majibu hayo, Muhammad (S.A.W) akasema:

Zaid, unafahamu ni kwa kiasi gani ninakupenda. Wakati huohuo hapa kuna baba yako na baba yako mkubwa. Wamekuja hapa kukuchukua. Unaweza kubaki hapa ikiwa unataka kubaki au unaweza kuondoka nao ikiwa utapenda. Uko huru kuchagua.

Zaid akamtazama baba yake na baba yake mkubwa kisha akasema kwa moyo mkunjufu:

Ninataka kubaki na wewe. Kwangu mimi wewe una thamani kama mama, baba na baba mkubwa.

Baba yake Zaid akashangazwa na maneno yale. Akamkaripia kwa kusema:

Unapendelea kuwa mtumwa mbele yetu? Zaid akamfuata baba yake na kumwambia:

Baba nimepata kila aina ya upendo kwa huyu baba na ninampenda sana. Nina furaha na amani kuwa naye. Tafadhali niache niishi naye.

Baada ya maneno hayo, baba yake Zaid hakuweza kuendelea kumlazimisha Zaid. Hakutaka kupoteza furaha ya mtoto wake. Hivyo, alimwacha abaki pale. Alijua atakuja kumtembelea mwanaye wakati wowote akitaka. Alifarijika kumwacha mwanaye akilelewa na mtu mwenye upendo kiasi kile.



KIJANA ALIYEPENDWA NA MTUME (S.A.W)

Zaid alikuwa katika maadili sahihi ya Uislam chini ya uangalizi wa Mtume (S.A.W). Aliyatoa maisha yake katika dini ya Mwenyezi Mungu. Alitumia muda wake katika kutetea dini ya Uislam na baadaye aliuawa akiwa vitani. Mtume wetu (S.A.W) alifurahi kwa kuwa Zaid alipata bahati ya kufariki kama shahidi akipigania dini ya Mwenyezi Mungu lakini alikuwa na huzuni kwa kumpoteza kijana wake. Alikwenda nyumbani kwa Zaid kuwafariji mke na watoto. Mtoto mdogo wa Zaid aitwaye Usama alikuwa akilia kwa kumpoteza baba yake. Mtume wa Mwenyezi Mungu wakati wote alikuwa akiwajali yatima. Kuanzia siku hiyo hakumuacha Usama peke yake. Mtoto huyu mwerevu alikua chini ya mapenzi na malezi ya Mtume (S.A.W).

Mtume wa Mwenyezi Mungu alimlea Usama kama anavyowalea wajukuu zake. Alikuwa akimuweka Hassan katika goti lake moja na Usama katika goti jingine akiwabusu na kuwapapasa.

Siku moja Usama (r.a) alijikwaa kwenye kizingiti cha mlango na kudondoka. Akaumia usoni. Mtume akamwambia mkewe Aisha aufute uso wa Usama. Pale ambapo mama yetu Aisha alionekana kuchelewa kidogo kumhudumia, Mtume wa Mwenyezi Mungu hakuweza kuvumilia. Alimkumbatia Usama na kumfuta kidonda chake. Hali hii ilimfanya Usama asahau maumivu aliyoyapata. Rafiki zake Usama walivyoshuhudia mapenzi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa Usama walimpa jina la "kijana anayependwa sana na Mtume (S.A.W).

Inawezekana vipi mtoto anayeishi katika nyumba yenye baraka kiasi hiki asiwe na furaha?



Kwa kuzingatia mapenzi ya dhati ya Mtume (S.A.W) mtoto Usama alisahau maumivu ya kumpoteza baba yake. Alimpenda sana Mtume na kumheshimu.

Usama alipofikia ujana, alienda na mtume kuufungua mji wa Makka pamoja na maswahaba wengine. Alishirikiana na mtume (S.A.W) katika kuangamiza masanamu. Usama hakubaki bila kufanya kazi. Alichukuwa ndoo ya maji na kufuta michoro yote iliyochorwa katika ukuta wa Alkaabah.

Baada ya miaka kadhaa kupita, Usama (r.a) akawa kijana shujaa mwenye imani. Mtume akamteua Usama kijana mwenye umri wa miaka 18 kuwa Kamanda wa Jeshi la Waislamu.

Kuanzia wakati huo Usama akawa shujaa wa Uislamu, alishiriki vita moja baada ya nyingine.

HASSAN NA HUSSEIN (R.A)

Mtume wetu mpendwa alikuwa na wajukuu wawili ambao ni Hassan na Hussein. Baba yao ni Ali (r.a) na mama yao ni Fatma (r.a). Mtume aliwapenda sana wajukuu wake hawa wawili. Alitoa maelezo kuhusu wajukuu wake hawa akasema "watoto hawa wawili kwangu mimi ni kama ua la waridi katika ulimwengu huu" Alikuwa akiwatembalea mara nydingi na wakati mwingine watoto hao walikuwa wakimtembelea babu yao. Wanapokuwa pamoja, Mtume (S.A.W) hucheza nao. Alikuwa akiwabeba mgongoni huku akiwaburudisha kwa kusema "mmepata mbebaji mzuri na ninyi mmekuwa waongozaji wazuri"

Siku moja mtume alikuwa akiwaswalisha maswahaba zake msikitini (Swahaba maana yake ni mfuasi wa Mtume (S.A.W) aliyekuwa karibu naye zaidi wakati wa kutangaza dini), mara Hassan na Hussein wakatokea msikitini. Walikuwa wakimwangalia babu yao kwa macho ya udadisi. Walipomwona anaongoza swala mbele ya maamuma wakaenda karibu yake huku wakimtazama. Mtume (S.A.W) alipokuwa anasujudu, maswahaba zake pia wakasujudu. Hassan na Hussein walipomwona babu yao anasujudu wakamrukia mgongoni kwa furaha wakaanza kucheza.



Kama mtume (S.A.W) angesimama kutoka katika sijida, Hassan na Hussein wangeanguka chini. Ndipo Mtume akarefusha muda wa kusujudu akiwasubiri washuke chini kutoka mgongoni walipokuwa wakicheza.

Watoto hawa wadogo hawakufahamu kwamba wanazuia swala kuendelea. Baada ya kucheza kwa muda walishuka kutoka katika mgongo wa babu yao. Mtume (S.A.W) akasimama na kuendelea na swala.

Baada ya swala kumalizika maswahaba wakamuuliza Mtume (S.A.W) sababu ya kurefusha swala, kisha Mtume (S.A.W) akajibu:

Wajukuu zangu walipanda mgongoni wakati wa kusujudu nikahofia kuwadondosha endapo ninginuka, hivyo nikaamua kurufusha muda wa kusujudu.

Kisa hiki kinaonesha ni kwa namna gani Mtume wa Mwenyezi Mungu alivyokuwa akiwapenda watoto. Ni kwa namna gani Hassan na Hussein (r.a) walikuwa na furaha kwa kumpata babu ambaye alikuwa akiwapenda sana. Walikuwa na bahati kiasi gani. Sivyo?



NANI ALIKUWA WA KWANZA KUOMBA MAJI?

*M*tume wa Mwenyezi Mungu alitaka Hassan na Hussein wawe Waislamu wazuri. Wakati wote alikuwa akiwaongoza kuwa watu wema na wenye huruma. Pamoja na hayo alishiriki nao michezo mbalimbali kama vile miereka na riadha ili kuwafanya kuwa imara na wenye afya. Watoto hawa wawili waliokuwa kama waridi kwa Mtume (S.A.W), daima hawakuoneana wivu walipokuwa wakitekeleza ushauri wa babu yao hivyo, walishirikiana vyema.

Siku moja Mtume (S.A.W) alikwenda kuwatemebelea wajukuu zake kama ilivyokuwa kawaida yake. Ilipofika jioni Hassan na Hussein hawakutaka kumruhusu aondoke. Walitaka waendelee kuwa naye. Mtume (S.A.W) hakupingana na matakwa ya wajukuu zake. Usiku alikwenda kulala Hassan akiwa upande mmoja na Hussein akiwa upande mwagine. Usiku wa manane wakiwa wamelala Hassan aliamka na kumwomba babu yake maji ya kunywa. Mtume aliamka mara moja akamimina maji kwenye kikombe kisha akampa Hassan. Muda mfupi baadaye Hussein naye akaamka na kuomba maji ya kunywa. Mtume akaweka maji katika gilasi nyingine na kumpatia Hussein.

Fatma (r.a) alipoona akamuuliza baba yake:

Ewe baba yangu, umempa Hassan maji kwanza, je ni kwa kuwa unampenda zaidi?

Mtume (r.a) alijibu, hapana, Hassan alikuwa wa kwanza kuomba maji ndiyo sababu nikaanza kumpa yeye.



Mtume wa Mwenyezi Mungu hakuwabagua watoto hata kama wasinge kuwa wajukuu zake. Aliwajali wote kwa uadilifu na usawa. Kitendo cha kumpa Hassan maji kwanza kinamfundisha Hussein kuwa mpole na kuheshimu haki za kaka yake. Matendo yote aliyofanya Mtume (S.A.W) huwa na mafunzo mahususi kwetu.





ANAS (R.A) MVULANA ALIYETUNZA SIRI

*A*nas (r.a) ni mionganini mwa watoto wema waliopata bahati ya kulelewa na Mtume (S.A.W). Baada ya Mtume (S.A.W) kuhamia Madina mama yake Anas alimpeleka mwanaye kwa Mtume (S.A.W).

- Mama yake Anas alisema kumwambia Mtume (S.A.W), Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, ulipokuja Madina kila mmoja amekupatia zawadi. Kwa kuwa mimi ni mwanamke fukara, sina cha kukupa. Huyu hapa ni mtoto wangu. Ninakupatia akusaidie majukumu yako.



Mtume (S.A.W) alifurahishwa sana na ukarimu wa huyu mama. Alimwangalia mtoto Anas ambaye alikuwa akitazama kwa macho ya furaha. Ni dhahiri kwamba alitaka kuishi na Mtume (S.A.W). Hakuna ambaye anaweza kumkataa mtoto mwerevu kiasi hiki! Mtume (S.A.W) hakukataa hisani aliyofanyiwa hivyo, alikuwa tayari kumpokea Anas.

Siku zilipita na mtoto Anas akaendelea kukua chini uangalizi na mapenzi ya Mtume huku akiwa na furaha katika maisha yake.

Siku moja Mtume (S.A.W) alimuagiza Anas (r.a) mahali fulani. Anas (r.a) akaondoka mara moja. Hata hivyo, alipoona watoto wenzake wanacheza barabarani akasahau kuwa ameagizwa akaanza kucheza na wenzake. Mtume (S.A.W) akawa na wasiwasi baada ya kuona muda umepita na Anas (r.a) hajarejea nyumbani. Alitoka nje na kuanza kumtafuta. Baada ya muda mfupi akamwona Anas (r.a) akiwa anacheza na marafiki zake. Alikwenda karibu yake na kumuuliza kwa upole.

- Ewe Anas! Umekwenda nilipokuagiza?
- Anas (r.a) alipomwona Mtume (S.A.W) akakumbuka kwamba alikuwa ameagizwa. Aliona aibu kwa kile alichokifanya, akasema.
- Ninakwenda sasa hivi Mtume wangu mpendwa. Akakimbia na kupotea katika eneo lile.
- Usiku Anas (r.a) akarejea nyumbani akiwa amefanya kazi aliyoelekezwa. Akamjulisha Mtume (S.A.W) kisha akaenda chumbani kwake. Mama yake alipomwona akamuuliza Anas (r.a)
- Kwa nini umechelewa sana mwanangu mzuri?
- Anas (r.a) akajibu, Mtume (S.A.W) aliniagiza.
- Mama yake akamuuliza, Mtume (S.A.W) alikuagiza wapi?
- Anas akajibu kwa haraka.
- Mama yangu, hii ni siri baina ya Mtume (S.A.W) na mimi. Siwezi kueleza siri hii kwa mtu yeyote.
- Maneno ya Anas (r.a) yalimfurahisha mama yake, akamwambia:
- Umeefanya vizuri Anas. Usieleze siri ya Mtume (S.A.W) kwa mtu yeyote.
- Kutunza siri ni tabia njema. Na inapokuwa ni kutunza siri ya Mtume (S.A.W) linakuwa ni jambo bora kuliko kitu kingine chochote. Ni furaha iliyoje kwa Anas (r.a) kufahamu jambo hili katika umri mdogo?

MTOTO WA KWANZA KATIKA UISLAMU

*M*akka ni eneo lenye joto kali sana. Wakati mwingine miezi mingi ilipita bila ya kuwa na mvua, hali ambayo ilisababisha ukame. Katika kipindi hicho watu hupata shida ya njaa. Siku moja wakati wa njaa alitokea fukara mmoja katika nyumba ya baba mdogo wa Mtume, Abu Talib. Alikuwa katika wakati mgumu wa kuwahudumia watoto wake sita. Mtume aliwapenda sana ndugu zake. Alimfanya hisani baba yake mdogo kwa kumchukua mmoja wa kaka zake. Kuanzia siku hiyo, kaka yake Mtume (S.A.W) Ali akaishi katika nyumba ya Mtume akiwa sambamba na Mtume. Ali alimpenda sana kaka yake Muhammad (S.A.W) ambaye hakuwahi kumkasirikia na wakati wote alimlea kwa mapenzi.

Miaka mingi ikapita. Ililiwa ni kipindi ambacho Mtume anapata taarifa za utume wake. Siku hiyo Mtume (S.A.W) aliwa akiswali na mkewe Khadija (r.a). Wote wawili walionekana kuwa na amani na furaha wakati wa ibada. Ali alifurahishwa sana alipowaona. Akawasubiri kwa utulivu wamalize kuswali. Kisha akawaauliza:

- Mlikuwa mnafanya nini?

Mtume (S.A.W) akamkumbatia kwa taratibu.

- Ali tazama, kile ulichokiona ni ibada ya swala. Kwa kufanya hivyo, tunamuabudu Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu ameniteua kuwa Mtume na ninakuusia uungane nasi kumuabudu.




Baada ya kutafakari maneno yale kwa muda kwa kuwa ilikuwa ni mara yake ya kwanza kuyasikia, akajibu kwa hisia:

- Siwezi kusema lolote kabla ya kumuuliza baba yangu.
- Mtume (S.A.W) akamwambia Ali (r.a), ikiwa utapenda unaweza kufanya kile nilichosema. Lakini ikiwa hauko tayari tafadhalii tunza siri hii. Usimwambie mtu yeoyote.
- Mtume (S.A.W) alisema maneno hayo kwa Ali kuashiria kwamba bado hajaanza rasmi kuwaita watu katika Uislamu.

Ali (r.a) alifikiri usiku kucha. Alikuwa na mapenzi ya dhati kwa Mtume (S.A.W) ambaye hajawahi kufanya mambo mabaya. Hakuwa na shaka kwamba mambo aliyokuwa akieleza Mtume (S.A.W) ni ya kweli. Alimwendea Mtume (S.A.W) na kumwambia:

- Mwenyezi Mungu hakumuuliza mtu yeoyote alipokuwa akiniumba. Ni kwa nini mimi nimuulize mtu kwamba nimwabudu Mwenyezi Mungu au la?

Baada ya kusema maneno haya Ali (r.a) akatoa shahada na akawa mionganii mwa watu wa mwanzo kuamini Uislamu. Alikuwa ni mtoto wa kwanza kuukubali Uislamu. Ni furaha iliyoje kwa Ali na watoto wenzake wote Waislamu?



MVULANA ALIYERUSHASHA MAWE KWENYE MITI YA TENDE

Kama nikiwa uliza ni tunda gani zuri sana linalopandwa Madina nina uhakika kwamba wote mtasema tende. Ndiyo, Mji huu mtakatifu ambao Mtume wetu alihamia ni maarufu kwa miti ya tende. Huchanua kama mwavuli mkubwa na kulipamba anga la Madina. Tende hukomaa wakati wa majira ya joto. Huwa tamu sana. Watoto wa Makka wanapenda sana tende.

Rafi ni miongoni mwa watoto wanaopenda tende. Siku moja Rafi alikuwa barabarani anacheza na marafiki zake. Baada ya kucheza kwa muda kidogo marafiki zake walienda nyumbani. Lakini Rafi hakutaka kwenda nyumbani. Akaanza kutembea, baada ya muda mfupi, akaona tende katika mti uliokuwa katika shamba la tende. Mmmm! Tende hizo zilizoiva zilionekana zitakuwa ni tamu sana. Akamua kuingia katika shamba. Akachukua mawe na kuanza kuangua tende.

Baada ya muda kidogo tende mojamoja ikaanza kudondoka





kutoka kwenye mti. Rafi aliokota tende kwa furaha. Alikaa chini ya mti na kuanza kula. Mmm! Tende zilikuwa tamu sana kwa hiyo kadiri alivyokuwa anakula ndivyo alivyokuwa akipata hamu ya kula zaidi. Baada ya muda kidogo kupita ilisikika sauti ikitokea katika miti:

- Wewe mtoto! Unafanya nini hapo?

Rafi aliogopa alipoona mtu anakimbia kuelekea alipokuwa.

- Uhmm! Ninachuma tende , Rafi alimwambia yule mtu.
- Ooh! Vizuri. Je, uliomba ruhusa ya kuchuma tende kwa mwenye shamba hili. Hizi ni tende zangu!

Yule mtu alimwambia hivyo huku amemshika Rafi mkono na wakatoka pale shambani.

- Twende, ninakupeleka kwa Mtume (S.A.W).

Kisha walifika msikitini. Yule mtu akamwambia Mtume (S.A.W) kilichotokea. Rafi alisubiria. Mtume (S.A.W) akamwita Rafi na kumuuliza:

- Oh! Mwanangu, ni kwa nini ulirusha mawe kwenye mti wa tende? Rafi alijibu kwa sauti ya kutetemeka:
- Nilikuwa nina njaa, sikuweza kuvumilia nilipoona tende. Mtume alimwonea huruma mtoto huyu ambaye alionekana hatambui kosa.
- Mtume akamwambia, mwanangu, usiingie kwenye shamba lolote bila kuomba ruhusa kwa mwenye shamba. Vilevile, unaweza kula tende ambazo tayari zimeshadondoka chini ya mti.

Sauti ya huruma ya Mtume (S.A.W) ikamfanya Rafi ahisi upendo wa Mtume wa Mwenyezi Mungu ambaye alimuonya kwa upendo.

- Mtume wangu ninaahidi sitarudia tena. Alisema Rafi. Mtume (S.A.W) alimwombea Rafi dua kwa kusema:
- Eee Mwenyezi Mungu ninakuomba umpe mvulana huyu chakula.

Siku hiyo Rafi akamwomba msamaha mwenye shamba. Tangu siku hiyo hakuingia tena kwenye shamba bila kuomba ruhusa kwa mwenye shamba.



MSICHANA MDOGO YATIMA

A subuhi moja ya siku ya sherehe, mitaa ya Madina ilijaa watoto wenyewe sauti ya uchangamfu. Mtume alikuwa nje ya nyumba yake akiangalia namna watoto wanavyofurahia. Muda huohuo akamwona msichana ambaye analia kwa sauti ya chini katika kona. Alijiuliza msichana huyu ana shida gani? Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.A.W) alienda alipokuwa mtoto na kumuuliza:

- Mwanangu, ni kwa nini unalia katika siku nzuri kama hii ya kushereheke?



Msichana huyo mdogo akajibu bila kuinua kichwa chake:

- Katika sherehe iliopita baba yangu alikuwa na sisi, lakini sasa hayupo tena. Katika vita vya mwisho alipigana pamoja na Mtume (S.A.W) na alifariki. Nimemkumbuka sana. Mtu yeyote anaweza kulia akiwa yatima.

Mtume alihuzunishwa sana na maneno ya mtoto huyo. Alimpapasa kichwa chake na kumwambia:

- Ooh!, Mwanangu, futa machozi yako. Je, utapenda Mtume awe baba yako? Fatma (r.a) awe dada yako na Aisha (r.a) awe mama yako?

Yule mtoto akainua kichwa chake taratibu, baada ya kusikia maneno haya yaliyoupa faraja moyo wake. Alipomwona mtu aliyejikuwa akizungumza naye aligundua kwamba ni Mtume (S.A.W). Ghafla akaacha kulia. Ni mtoto gani atakayekataa ombi zuri kama hilo la Mtume (S.A.W)? Mtume (S.A.W) aliushika mkono wa msichana yule na kuondoka naye.

Walipofika nyumbani, Mtume (S.A.W) alimtambulisha yule mtoto kwa mke wake Aisha (r.a) na kwa mwanawe Fatma (r.a). Wao pia walimpenda mgeni wao. Walimnawisha mikono na uso. Wakamvalisha nguo mpya. Wakamwandalia chakula kizuri na kumlisha. Kisha walimpa fedha kidogo na kumpeleka nje akacheze na wenzake. Yule msichana alikuwa na furaha sana.

Watoto waliokuwa wakicheza nje walishangaa walipomwona amevaa nguo mpya na ana uso wa furaha.

- Walimuuliza, nini kimetokea?
- Yule msichana akawajibu, na mimi nina baba sasa. Pia, ni baba mzuri hakuna anayeweza kufanana naye katika hii dunia. Aisha (r.a) ni mama yangu, Fatma (r.a) ni dada yangu, ananipenda na amenivalisha hizi nguo mpya. Ni nani asingefurahi kuwa na familia bora kama hii? Ndiyo maana nina furaha sana.

Kwa mara nyingine, Mtume (S.A.W) akamfanya yatima awe na furaha. Furaha ya yule msichana mdogo ikawa furaha ya watoto wengine. Kisha wakaanza kucheza pamoja.



MTU MWAMINIFU ZAIDI

A Ika'aba nyumba ya Mwenyezi Mungu imeharibiwa na mvua ya miaka mingi. Kuta zake zilitikiswa na kupata nyufa kwa sababu ya mafuriko ya hivi karibuni. Watu wa Makka walipata pigo. Walitaka kuilinda nyumba ya Mwenyezi Mungu kwa kuijenga tena. Walikutana pamoja na kuelezana jukumu la kuijenga Alka'aba. Kutokana na uamuzi uliofikiwa kila ukoo ultakiwa kujenga sehemu ya Alka'aba ili kila mmoja atekelze wajibu wake. Vifaa vya ujenzi vilisambazwa na ujenzi wa Alka'aba ulianza.

Kila ukoo ultarajiwa kukamilisha jukumu lake. Hivyo, ujenzi wa Alka'aba ulikamilika kwa muda mfupi.

Ulfika wakati wa kuweka Jiwe jeusi la Alka'aba sehemu yake. Jiwe jeusi la Alka'aba linalindwa tangu enzi za Mtume Ibrahim na mwanaye Ismail walipojenga Alka'aba. Kwa sababu hii kila mkuu wa ukoo alitaka jiwe hilo liwekwe kwenye eneo lake. Hawakuweza kukubaliana. Kwa hiyo walikuwa na hasira na wakaanza kugombana. Walikaribia kutoa jambia zao na kupigana ndipo mtu mmoja mionganoni mwao akasema:

- Subirini! Hakuna sababu ya kugombana. Ni vizuri tukachagua msuluhishi wa suala hili mionganoni mwetu.

Walikubaliana na wazo hilo. Hata hivyo hawakujuu ni nani wanayeweza kumchagua kwa sababu walikuwa hawaaminiani. Hatimaye waliamua kwamba mtu wa kwanza kuingia getini siku inayofuata watamchagua kama msuluhishi. Asubuhi na mapema ya



siku inayofuata kila mmoja alienda kwenye Alka'aba na kuanza kusubiri kuona mtu wa kwanza kuingia katika mageti.

Kisha Mtume Muhammad (S.A.W) alionekana katika geti. Aliwasalimia na kuingia. Baada ya kumwona mtume (S.A.W) anakuja, mtu mmoja akasema kwa furaha:

- Muhammad huyo anakuja!

Kila mmoja alimuangalia Mtume kwa mshangao. Muhammad ni mwaminifu. "Kila moja alikuwa na furaha kwamba yeye ndiye atakayeingia Alkaaba. Walimwambia kuhusu mzozo wao na walitaka awe msuluhihi. Mtume (S.A.W) alikubali wazo lao kwa furaha. Akawaomba wampe kipande cha kitambaa kisha akaweka jiwe jeusi katika kitambaa hicho na kumwambia kila kiongozi wa ukoo kushika kona ya kitambaa hicho. Kwa namna hii jiwe liliwekwa kwenye sehemu yake na kila mtu na kisha Mtume akatoa jiwe kwenye kitambaa na kuliweka katika sehemu yake katika Alka'aba.

Kwa kufanya hivi Mtume (S.A.W) alitatua tatizo kabla halijawa kubwa na kila mtu aliridhika.



HUZUNI YA FATMA

A Ikaaba ilikuwa sehemu ambayo Mtume wetu (S.A.W) aliipenda sana. Alipenda kumwabudu Mwenyezi Mungu katika hiyo nyumba ya Mwenyezi Mungu ambayo inaonekana kama lulu nyeusi katikati ya Makka.

Mpaka sasa Alka'aba ni sehemu ya kukutana Waislamu wote duniani. Kukutana Alka'aba, kuswali na kuabudu pamoja ni furaha kubwa sana kwa Waislamu.

Siku moja Mtume wetu (S.A.W) alikuwa anaswali kwa unyenyekevu katika nyumba ya Mwenyezi Mungu. Alikuwa anamwomba Mwenyezi Mungu kwa moyo wake wote watu waache kuabudu sanamu na wamwabudu Mwenyezi Mungu.

Wakati huo, Abu Jahl, adui mkubwa wa Uislamu pamoja na marafiki zake walikuwa wame-kaa karibu na Alka'aba.



Utulivu wa Mtume wakati wa kuswali ulimkera Abu Jahl akaanza kulalamika kwa kusema: "Muhammad anathubutuje kufanya ibada hapa?"

Alikuwa anaogopa kwamba watu watavutiwa na Muhammad (S.A.W) na kuwa Waislamu. Hofu yake ilimfanya apate wivu, harakaharaka akapanga mpango wa kuharibu swala ya Mtume na kuuliza:

- Ni nani kati yenu anaweza kuweka utumbo wa ngamia katika mgongo wa Mtume wakati anaswali? Mtu mmoja mwenye roho mbaya kuliko wote kati yao akasema kwa sauti:

- Ninaweza. Nipe mimi hiyo kazi. Nitaifanya mimi!

Kisha akakimbia kutafuta utumbo wa ngamia aliyechinjwa muda si mrefu. Muhammad alikuwa anaendelea kuswali na alikuwa hajui kinachoendelea. Yule mtu akamkaribia Mtume taratibu na kuweka utumbo wa ngamia katika mgongo wake wakati alipokuwa anasujudu. Abu Jahl na marafiki zake walioona lile tukio wakaanza kucheka kwa sauti...

Mtume akaendelea kusujudu huku akiwa na utumbo wa ngamia mgongoni. Watu walioona tukio hili walikimbia kumwambia Fatma (r.a) ambaye ni binti wa mtume. Fatma (r.a) hakuamini alichosikia na harakaharaka akakimbia kuelekea Alka'aba akiwa na huzuni. Macho yake yakajawa na machozi ya huzuni. Alichukua ule utumbo katika mgongo wa baba yake na kuutoa.

Mtume akamaliza swala yake kwa unyenyekevu. Kisha alimkumbatia mtoto wake na kumfuta machozi yake. Kisha akamwangalia Abu Jahl na marafiki zake na kusema:

- Ooh! Mwenyezi Mungu unajua utakachokifanya kwao!

Baba na mtoto wake wakashikana mikono na kuondoka kuelekea nyumbani. Mtume wetu hakukasirika wala hakuwagombeza kwa walichomfanyia. Mara zote aliwajibu kwa busara na mara zote dua zake zilikuwa zinakubaliwa.



SAHIL NA KAKA YAKE SUHAIL

*M*sume baada ya kuhamia Madina alitaka kujenga msikiti kwa ajili ya Waislamu kuswalia. Siku aliyokuwa anahama, ngamia wake anayeitwa Qaswah aliinama chini na kukaa ardhini na kupumzika. Aridhi hiyo ilikuwa inamilikiwa na vijana wawili wa kiume ambao ni yatima Sahi na Suahil ambao walikuwa wanatumia ardhi hiyo kukaushia tende. Mtume (S.A.W) alitaka kuinunua hiyo ardhi ili ajenge msikiti kwa hiyo aliwaita Sahl na Suahil. Ndugu hao wawili walienda kwa Mtume (S.A.W) haraka. Aliwaeleza wazo lake na kuwaomba wamuuzie hiyo ardhi. Lakini badala ya kuuza ardhi hiyo, Sahil na Suhail waliamua kumpa Mtume (S.A.W) hiyo ardhi kama zawadi. Mtume alikataa kupewa ardhi hiyo bure na vijana hao wawili hivyo akainunua.

Kisha furaha ikaenea katika ardhi hiyo. Maswahaba wa Mtume wakafanya usafi katika ardhi hiyo, wakabeba mawe na mchanga wakaanza kutengeneza matofali. Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.A.W) aliweka tofali la kwanza la ujenzi wa msikiti huo pamoja na Abu Bakari (r.a), Umar (r.a), Othman (r.a) na Ali (r.a). Kwa hiyo, msingi wa msikiti ulijengwa na maswahaba wa Mtume (S.A.W)

Ujenzi wa msikiti uliendelea bila kupumzika. Mtume (S.A.W) pia alikuwa anafanya kazi ya ujenzi. Maswahaba zake walipomwona akibeba matofali mazito walimwambia "Tuache tukusaidie" lakini Mtume hakukubali, na alionekana kuwa na juhudhi kiasi kwamba maswahaba zake waliendelea kufanya kazi kwa bidii.

Ujenzi wa msikiti ukakamilika kwa kipindi kifupi. Sahl na kaka yake Suhail walikuwa na furaha sana na walijivunia kwa sababu msikiti kwa ajili ya Waislamu kuswalil ulikuwa



umejengwa katika ardhi yao. Waliuita msikiti huo Al-Masjid al-Nabawi yaani "Msikiti wa Mtume".

Tangu wakati huo kukawa na msikiti kwa ajili ya Waislamu kufanya ibada zao kwa furaha. Vilevile, katika eneo hilo waliweza kumwona Mtume (S.A.W) kila walipotaka kumwona na kujifunza misingi ya Uislamu kutoka kwake. Pia, masuala muhimu yaliweza kujadiliwa na uamuzi ulifanyika katika msikiti huo. Msikiti huu pia ulikuwa sawa na nyumba kwa Waislamu na sehemu ya kukutana.

Msikiti wa Mtume ni miuongoni mwa misikiti mizuri duniani kote ambao ulijengwa kwa ushirikiano wa Waislamu. Mpaka sasa unaendelea kutumiwa na Waislamu wote. Watu wamekuwa wakiswali na kuabudu katika msikiti huo kwa karne nyingi. Msikiti wa Mtume una kumbukumbu nzuri za utukufu wa Mtume (S.A.W).

Sahl na kaka yake Suhail wanafuraha isiyo kifani kwa ardhi yao kuwa na msikiti mzuri!





UTUKUFU WA WITO WA ADHANA

*J*angu wakati huo Waislamu walikuwa na msiki na ambao waliutumia kuswali pamoja. Kulikuwa na marafiki wengi ambao walikuwa wanakusanyika pamoja kwa ajili ya kuswali.

Kuswali kwa mkusanyiko lilikuwa jambo kubwa lakini kulikuwa na ugumu wa kufahamu na kutofautisha muda wa kuswali.

Kutokana na tatizo hili wakati mwagine waumini walifika kwenye swala kwa kuchelewa na kukosa swala ya pamoja na wakati mwagine walifika mapema sana na iliwabidi wasubiri.



Mtume (S.A.W) alitaka kutatua tatizo hili na aliwaomba waumini watoe maoni. Baadhi yao walisema:

- Tunaweza kugonga kengele kama wanavyofanya Wakristo.
- Tunaweza kupiga tarumbeta kama wanavyofanya Wayahudi.
- Na baadhi yao walisema:
- Tunaweza kuwasha moto mkubwa.

Mtume (S.A.W) hakukubali maoni haya kwa sababu yalifanana na wito wa madhehebu mengine. Alitaka wito wa swala wa kipekee. Siku ziliendelea kupita na siku moja muumini alienda kwa Mtume (S.A.W) na kumwambia:

- Mtume wa Mwenyezi Mungu, nimeota ndoto ya namna ya kuwaita waumini katika swala na kumwelezea Mtume ndoto yake.

Mtume aliipenda ndoto hiyo na kusema "Mwenyezi Mungu amependa, ni ndoto ya kweli. Mfundishe Bilal (r.a) maneno uliyoyaota katika ndoto yako na mwambie ayatamke:"

Alienda kwa Bilal (r.a) na kumfundisha maneno aliyoyaota kwenye ndoto yake.

Bilal, (r.a) ambaye alikuwa na sauti nzuri alipanda sehemu ya juu na kuanza kuyasema maneno hayo aliyojifunza:

Allahu Akbar, Allahu Akbar, (Mwenyezi Mungu Mkubwa, Mwenyezi Mungu Mkubwa),

Ashhadu an la ilaha illa illah, (Hapana Mola apasaye kuabudiwa ila Mwenyezi Mungu pekee),

Ashhadu anna Muhammadan Rasulullah, (Na Muhammad ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu)

Hayya 'ala's-salah, hayya 'ala's-salah, (Njooni katika swala, njooni katika swala)

Hayya 'ala'l-falah, hayya 'ala'l-falah, (Njooni katika ufaulu, njooni katika ufaulu)

Allahu akbar, Allahu akbar, (Mwenyezi Mungu Mkubwa, Mwenyezi Mungu Mkubwa),

La ilaha illa'-Allah, (Hapana Mola apasaye kuabudiwa ila Mwenyezi Mungu pekee),

Kwa hiyo Waislamu walipata namna nzuri kama wanavyofanya katika masuala yao mengine kwa kuwa walikuwa na mtume ambaye aliwapenda na mara zote aliwafundisha yaliyo mema. Adhana ina utukufu kiasi gani kwa Waislamu?

FURAHYA MTUMWA

*H*apo zamani kulikuwa na mwanaume aliyeitwa Abu Masud (r.a). Siku moja alichukizwa sana na mtumwa wake na akamchapa sana. Kutokana na maumivu ya kuchapwa mtumwa alikuwa analia. Hasira za Abu Masud hazikuisha. Wakati huo sauti ilisikika ikiita:

- Abu Masud! Abu Masud!

Abu Masud (r.a) alikuwa na hasira sana kiasi kwamba hakusikia sauti iliyokuwa ikiita jina lake.

Aliendelea kumchapa mtumwa na sauti ilisikika tena ikiita:

- Abu Masud! Abu Masud! Laiti ungejua!

Aliposikia hii sauti Abu Masud (r.a) aligeuka nyuma. Alimwona Mtume wetu (S.A.W) anamwangalia.

Abu Masud aligeuka kuwa mwekundu kutokana na hasira. Alijawa na wasiwasi na hakujua cha kufanya. Alitikisa kichwa chake kutokana na hasira na kusubiri.

"Daah!" akaanza kujilaumu, Mtume ameshuhudia kitendo kibaya kilichofanyika kwa mtu dhaifu. Natamani ningedhibiti hasira zangu na kutokumchapa mtumwa huyu masikini:



Mtume (S.A.W) kwa huruma alimkaribia yule mtumwa aliyeokuwa na maumivu, na kumgeukia Abu Masud na kumwambia:

- Ewe, Abu Masud! Laiti ungejua kwamba Mwenyezi Mungu ana nguvu kubwa kwako kuliko ulioitumia kwa mtumwa huyu.

Abu Masud (r.a) alikuwa ameshagundua kosa lake. Huzuni yake ikaongezeka zaidi kutokana na maneno ya Mtume (S.A.W). Akamwambia Mtume (S.A.W) ili kurekebisha kosa lake:

- Mtume wangu mpPENDWA! Mwachilie mtumwa
huyu awe huru kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.
Ninaahidi sitarudia tena kumfanyia mtu yeyote
nilichofanya leo!

Mtume (S.A.W) alitabasamu.
Alifurahi kwamba Abu Masud (r.a)
amegundua makosa yake.
Mtumwa aliyeokuwa na
maumivu kwa sababu
ya kuchapwa alikuwa
na furaha pia. Furaha ya
kuachiliwa huru ilimfanya
ahisi amezaliwa upya.

Mtume wetu mpPENDWA
mara zote amekuwa akiwatetea
wanaodhulumiwa. Alikuwa Mtume wa
wale wenye njaa, kiu, maskini, waliokwama
na waliokosa msaada.

Alikuwa na moyo wa huruma kwa
kila mtu.




MTU MASKINI

*H*apo zamani palikuwa na mtu maskini aliyeishi Madina. Alikuwa maskini sana kiasi kwamba hakuwa na chakula nyumbani kwake. Yeye na familia yake walikuwa wanakabiliwa na tatizo la njaa na umaskini. Siku moja alienda kwa Mtume (S.A.W) na kumweleza tatizo hili.

Mtume (S.A.W) alimsikiliza mtu huyo kwa umakini. Baada ya mtu huyo kumaliza kuzungumza walikuwa na mazungumzo yafuatayo:

- Nyumbani kwako una nini?





- Ooh! Mtume wa Mwenyezi Mungu sina chochote isipokuwa kitambaa chakavu tunachokitumia kama tandiko na chupa ya maji.

- Nenda kaniletee nguo hiyo na hiyo chupa ya maji.

Yule mtu maskini alikimbia nyumbani kwake na kuchukua kitambaa na chupa ya maji na kumpelekea Mtume (S.A.W).

Mtume alichukua vitu hivyo na kuwaonyesha watu:

- Je, kuna mtu ye yeyote anayetaka kuvinunua?

- Mwanamume mmoja mionganoni mwa maswahaba akanunua vitu hivyo.

Mtume (S.A.W) alimpa yule maskini zile pesa.

- Mtume akamwambia "Nunua baadhi ya vyakula kwa ajili ya familia yako na zinazobakia nunua shoka kisha uniletee".

Yule mtu maskini alifanya kama alivyoelezwa na Mtume (S.A.W) na akarejea na shoka baada ya muda mfupi. Mtume alichukua shoka na kuliwekeea mpini. Kisha akampa yule mtu maskini lile shoka na kumwambia:

- Nenda kakate kuni msituni na uziuze. Uje kwangu baada ya siku kumi na tano unifahamishe maendeleo yako.

- Baada ya siku kumi na tano kupita mtu yule alivaa nguo mpya na kwenda kwa Mtume (S.A.W). Mtume alitabasamu na kufurahi alipomwona yule mtu.

- Mtume alimuuliza, unaendeleaje?

- Ooh! Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, Ninamshukuru Mwenyezi Mungu. Nimekata kuni mlimani kwa kutumia shoka langu, nikazipeleka sokoni na kuziwa. Nimepata pesa nyingi ndani ya siku kumi na tano. Nimeweza kupata mahitaji ya familia yangu kwa kutumia fedha hizo na nimejinunulia nguo mpya.

Mtume (S.A.W) alitabasamu na kumwambia yule mtu:

- Ni vyema kwako kukata kuni ili kukidhi mahitaji ya familia kuliko kuwa na alama ya omboomba katika sura yako Siku ya Kiama.

Yule mtu akamshukuru Mtume (S.A.W). Kutokana na mwongozo wa Mtume, alifanikiwa kuondokana na umaskini.

Tangu siku ile yule mtu hakuacha kukata kuni na kupata mali na aliishi maisha ya furaha na yenye amani.

ZAYD MWANDISHI KIJANA

*Z*alikuwa na yatima anayeitwa Zayd aliyeishi Madina. Baba yake Zayd alifariki ye ye akiwa na miaka sita. Zayd alikuwa kijana nadhifu. Alikuwa anaelewa na kutekeleza kila kitu anachoelekezwa. Hata hivyo alikuwa maskini kama ilivyokuwa kwa yatima wengine. Alikuwa anahitaji kuhudumiwa na kuonewa huruma. Miaka hiyo kulikuwa na vita kati ya Waislamu na watu wa Makka wanaoabudu miungu vilivyoitwa Vita vya Badri. Waislamu walishinda katika vita hivyo.

Kisha Mtume (S.A.W) akawaeleza mateka wa Makka:

- Yeyote atakayefundisha watoto 10 wa Madina kusoma na kuandika ataachiliwa huru!
- Baada ya siku hiyo watoto wa Madina wakaanza kusoma.

Zayd akawa mionganoni mwa watu waliojifunza kusoma na kuandika kwa muda mfupi. Kijana huyu mdogo akaanza kusoma Kur'an muda mfupi tu baada ya kujua kusoma. Alijiwekea malengo ya kusoma sura kadhaa za Kur'an kwa kipindi kifupi. Kijana huyu mwerevu alipelekwa kwa Mtume (S.A.W).

Mtume (S.A.W) akatabasamu na kumuuliza:

- Unaitwa nani?



- Ninaitwa Zayd bin Thabit.
- Umehifadhi aya ngapi?
- Nimehifadhi sura 17.
- Unaweza kutusomea kidogo?
- Ndiyo ninaweza.

Zayd akasoma sehemu ya sura alizohifadhi. Hakukosea kabisa wakati wa kusoma. Usomaji wake ulikuwa unasikika vizuri na kwa usahihi. Mtume (S.A.W) alifurahishwa sana na usomaji wake na akataka ajifunze lugha ya kigeni. Wakati ule lugha kubwa ilikuwa lugha ya Kisirya. Zayd alifanya kazi kwa moyo wote tangu siku ile. Akajifunza lugha ya Kisirya kwa kipindi kifupi pamoja na kuimarika katika kuandika.

Baadaye Mtume (S.A.W) alimteua mtoto yule kuwa mwandishi wake. Kuanzia wakati ule ujumbe wa Mwenyezi Mungu kwenda nchi nyingine kwa lugha ya Kisirya ukaanza kuandikwa na Zayd. Baadaye Zayd alijifunza lugha nyingine na kuutumikia Uislamu katika maisha yake yote. Aliendeleza wazo la kukamilisha kusoma Qur'an.

Mtume (S.A.W) alikuwa anapenda kuwapa zawadi watoto wenye jitihada kama yeye. Hakuwahi kudharau maendeleo ya wato na wakati wote alikuwa akiwahamasisha kuwa na bidii.

Watoto wenye bidii kama Zayd (r.a) mara zote walizingatia ushauri wa Mtume (S.A.W) na hawakuwahi kuwa wavivu.



THALABA BIN HATIB ALIYEKUWA ANAOMBA UTAJIRI



*J*ahaba ni Muislamu aliyekuwa anaishi Madina, alitaka sana kuwa tajiri. Matamanio yake yalikuwa makubwa kiasi kwamba hakuwaza kitu kingine chochote.

Siku moja alienda kwa Mtume (S.A.W) na kumwambia:

- Mtume! Nimemwomba Mwenyezi Mungu niwe tajiri. Kutokana na ombi lake Mtume (S.A.W) alimwambia:
 - Ewe Thalaba! Mali kidogo ambayo unaweza kushukuru ni bora zaidi kuliko mali ambayo hutaweza kushukuru.

Baada ya maneno haya Thalaba aliondoka. Lakini, baada ya muda alirejea na kumsisitiza Mtume:

- Ooh Mtume wa Mwenyezi Mungu! Nimemwomba Mwenyezi Mungu anipe mali.

... Mtume wa Mwenyezi Mungu akamwambia:

- Ewe Thalaba! Hutaki kunitumia mimi kama mfano? Ninaapa kama ningetaka hii milima ya madini ya dhahabu na fedha ingeweza kugeuka na kuwa yangu.

Thalaba hakutaka kuelewa.

- Ninaapa kama utaniombea kwa Allah na akanipa mimi mali, nitaheshimu haki ya kila mtu.

Baada ya Thalaba kusisitiza Mtume (S.A.W) alimwombea:

- Ee! Mwenyezi Mungu naomba umpe Thalaba mali nzuri.

Muda mfupi baada tu ya kuaomba, Mali ya Thalaba ikaanza kuongezeka na mifugo yake ikaanza kuongezeka kiasi kwamba ilibidi ahame eneo la mwanzo ili akakae sehemu ambayo mifugo yake itatoshea. Akaanza kuacha kwenda msikitini na kuwa mbali na Mtume (S.A.W) na Waislamu wengine.

Siku moja Mtume (S.A.W) kwa kuwa alikuwa hajamwona Thalaba msikitini kwa muda mrefu aliuliza:

Thalaba anaendeleaje? Maswahaba wakajibu:

- Thalaba amehamia bondeni. Haji kuswali kwa sababu ana mambo mengi ya kufanya. Mtume (S.A.W) akasema ninamwonea huruma Thalaba kwa kuacha kuswali. Mkumbusheni maneno haya aliyonieleza. "Kama nikiwa tajiri nitaheshimu haki ya kila mmoja". Maneno haya yamkumbushe wajibu wake wa kutoa sadaka.

Lakini Thalaba alikataa kutoa sadaka.

Akaacha kutoa sadaka kama alivyoacha kuswali.

Mtume (S.A.W) aliposikia kuhusu hili, uso wake ukajawa na huzuni na akasema:

- Ni aibu kubwa sana kwa anachofanya Thalaba. Ni huzuni kubwa!
- Thalaba amekuwa mtumwa wa mali yake.

Kama angesikiliza ushauri wa Mtume wetu mpendwa asingepotea kwa ajili ya vitu vyaa ulimwengu.

MTUME ALIPENDA SANA WATOTO

Mtume wetu Muhammad (S.A.W) alikuwa anapenda sana watoto. Alikuwa haachi kuwasalimia anapokutana nao, kuwapapasa vichwa vyao na kuwauliza kuhusu afya zao na matatizo yao. Wakati mwingine alikuwa akiwatania na wakati mwingine alicheza nao. Watoto pia walimpenda Mtume. Walipomuona walikusanyika pamoja na kumsalimia kwa kumshika mkono. Mtume (S.A.W) hakuwahi kuwachukiza na alimsikiliza kila mtoto. Alipenda kuwakumbatia na kuwabusu. Alipokuwa anazungumza na Hassan na Hussein (r.a) alikuwa anasema "Hawa ni maua yangu duniani.

Siku moja alikuwa amekaa msikitini, akawashika mkono Hassan na Hussein (r.a) na kuwabusu kwa upendo. Wakati huo mwanaume mmoja akaingia msikitini. Akamwona Mtume akizungumza na wajukuu zake na kusema:

- Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, nina watoto kumi na sijawahi kuwabusu kama unavyofanya wewe.

Mtume (S.A.W) ambaye alikuwa anashangazwa na namna mtu huyo asivyojali wala asivyokuwa na upendo kwa watoto wake ili kuonyesha kosa la mwanaume huyo alimwambia.

- Sasa mimi naweza kufanya nini kama Allah ameondoa huruma katika moyo wako?
- Kwa kusikiliza maneno hayo yule mwanaume akajawa na huzuni na kujuta kwa alichokuwa anafanya.

Mara zote Mtume (S.A.W) alikuwa akifanya jambo kwa ajili ya kuwajali watoto.



Siku moja katika mji wa Madina mama mmoja alikuwa akimwita mtoto wake ambaye alikuwa anacheza ili arejee nyumbani:

- Njoo, unajua ninataka kukupa nini? Mtume (S.A.W) ambaye alikuwa anawasikia aliuliza:
- Unataka kumpa nini mtoto wako?

Mama yule alipomwambia kwamba anataka kumpa tende, Mtume (S.A.W) alimwambia:

- Kuwa makini kama mtoto atakuja na hutampa kitu chochote utapata dhambi ya kudanganya.

Mtume (S.A.W) hakutaka watoto wawe na huzuni na hakuweza kuvumilia kuwaona wanalia. Hakuweza kuzuia upendo na kuwajali watoto. Mara zote watoto walikuwa wanaenda kwa Mtume kwa ajili ya kumweleza matatizo yao. Alikuwa Mtume wa wote, watoto, vijana na watu wazima.



USHUPAVU WA ABUU MAHZURAH (R.A)

*U*likuwa ni mwaka wa ushindi kwa Makka. Mtume wetu mpendwa (S.A.W) alikuwa anarejea kutoka Taif akiwa na marafiki zake. Alisimama Jiranah kufanya ibada. Mwadhini alianza kupiga adhana, Kikundi cha vijana wa Makka ambao hawakuwa Waislamu wakati ule, waliskia adhana. Wakajificha kwenye kona na kuanza kudhihaki adhana kwa kumuiga anayepiga adhana.

Mtume (S.A.W) akawasikia na kuwaita. Wale vijana wakaogopa kwa sababu walifikiri Mtume wa Mwenyezi Mungu angewakasirikia. Walienda kwa hofu. Mtume (S.A.W) alitabasamu na kuwauliza majina yao. Akamwambia kila mmoja apige adhana. Kila mmoja akapiga adhana kwa namna anavyojua. Mtume (S.A.W) aliwasikiliza na kumwambia Abou Muhzurah (r.a):

- Una sauti nzuri. Nenda kaadhini ili tuswali!

Abuu Muhzurah (r.a) hakuwa anajua namna ya kupiga adhana. Alimuiga tu mwadhini. Alipatwa na aibu, Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.A.W) bado alikuwa anatabasamu na aliadhini kisha akamsisitiza Abou Muhzura kwa kumwambia:



- Rudia adhana kama ninavyosema mimi. Abuu Mahzurah (r.a) alirudia maneno aliyoyasikia kwa bidii. Baada ya kurudia maneno hayo Mtume (S.A.W) akampa sarafu za fedha. Kisha akaweka mikono kwenye mabega yake na kumwombea. 'Mwenyezi Mungu akubariki na akupe radhi zake.

Ingawa Mahzurah (r.a) alitakiwa kuadhibiwa kwa kuigiza adhana. Lakini alishangazwa na ukarimu aliquofanyia Mtume (S.A.W) badala ya kumuadhibu. Ghafla akahisi kuwa na upendo mkubwa na Uislamu. Akaamini kwa moyo wake wote kwamba huyu ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Tangu siku hiyo akawa anapenda kujifunza adhana na akawa anamwuuliza Mtume (S.A.W):

- Je, unaweza kunithea mimi niadhini kama Muadhini wa Makka?

Mtume (S.A.W) alimkubalia ombi lake. Kuanzia siku hiyo Abou Muhzurah (r.a) akajifunza namna ya kuadhini kwa usahihi na akaanza kutoa adhana Al kaaba akisaidiana na Bilal al Habash.

Abou Mahzurah (r.a) aliendelea kuwa mwadhini katika kipindi cha maisha yake yote. Baada ya kifo chake warithi wake waliendelea kuadhini kwenye Al kaaba.

Kwa sababu ya uchangamfu na upendo wake Mtume S.A..W) alipendwa sana na watoto na vijana.

Bila shaka alifurahisha moyo wa Muhzura (r.a). Si ndiyo?



ZAWADI YA MSICHANA MDOGO

*M*tume wetu mpandwa (S.A.W) alikuwa anaishi vizuri na watu. Hakuwahi kukasirika na kumgombeza mtu yeyote aliyemuudhi. Alijitahidi watu wawe na furaha. Wakati mwingine aliwapa zawadi, na pia kuna wakati alipokea zawadi zao.



Watoto walimpenda sana Mtume wetu (S.A.W) na walipenda kutembea maeneo mbalimbali wakiwa naye, kwa sababu mara zote Mtume (S.A.W) aliwafanya wafurahi. Hakuwahi kula kitu chochote alicholetewa bila kuwagawia watoto.

Mtoto mmoja anayeitwa Saib alimtembelea Mtume (S.A.W) akiwa na rafiki zake na kumkuta Mtume anakula tende na waumini wake. Alipowaona watoto alitabasamu na kuwagawia kila mmoja tende. Sahib na marafiki zake wakafurahi na wakala tende kwa furaha.

Siku moja mama Rubeyyi aliweka tende na matango katika sahani na kumwambia msichana wake mdogo:

- Mtume (S.A.W) anapenda tende na matango. Mpelekee hizi tende na matango.

Yule msichana mdogo akazichukua kwa furaha na kuzipeleka kwa Mtume (S.A.W). Alipomkaribia akasema:

- Mama yangu amenitura nikuletee hizi tende na matango.

Kipindi kile Mfalme wa Bahrain alimpa Mtume (S.A.W) zawadi ya vito vyaya gharama. Mtume akaangalia sahani ya Rubeyyi. Aliipenda zawadi ya msichana huyo mdogo. Akachukua vito vilivyojaa kiganja chake alivyopewa na Mfalme wa Bahrain na kumpa yule msichana mdogo akisema:

- Chukua hii zawadi mwanangu.

Kwa sababu ya furaha yake, hakuju cha kufanya. Aliangalia vito vyake vyaya thamani na vyaya fedha vilivyojua mkononi mwake.

- Asante sana Mtume wangu (S.A.W), alishukuru na kukimbia harakaharaka kuelekea nyumbani kwao.

Furaha ya msichana huyo mdogo ikawa furaha ya Mtume (S.A.W). Kila mara aliwashauri waumini wake:

- Peaneni zawadi ili muongeze upendo baina yenu.

Mwislamu anayefuata ushauri wa Mtume ataendelea kutoa zawadi na kuwapenda wenzake.

MTUME ALIPENDA KUWA NADHIFU

*U*islamu unaweka msisitizo mkubwa katika usafi. Unawaelekeza waumini kuwa safi na kuhakikisha nguo zao ni safi, kupanga vitu vyao na kuweka nyumba zao katika mazingira ya usafi. Mtume wetu (S.A.W), pia alikuwa anatii maelekezo ya Allah. Aliweka msisitizo mkubwa katika kufanya usafi wa nguo zake, nywele na ndevu. Siku zote alipiga mswaki kwa mswaki uliotengenezwa kwa mti.

Siku moja Mtume (S.A.W) alikuwa anaenda msikitini. Ili kuwa nadhifu alijiangalia katika maji yaliyokuwa kwenye chombo na kufunga lemba lake. Akachana nywele na ndevu na kusema:

- Mwenyezi Mungu anawapenda waumini wake wanaovaa vizuri kwa ajili ya kuwatemebelea ndugu zao.

Kama ilivyokuwa kwa Mtume (S.A.W) maswahaba pia walikuwa wanapenda kuonekana nadhifu na hasa wanapokwenda msikitini ambapo huva nguo nzuri.



Siku moja kuna mtu alienda msikitini wakati Mtume yupo. Mtu huyo alionekana kama mtu aliyekurupuka. Ilionekana wazi kwamba hakujikagua wakati anatoka nyumbani. Mtume hakuupenda mwonekano wa mtu huyo. Akajaribu kumuuliza kwa namna ambayo haitamfanya ajihisi kudharauliwa:

- Je, una kitu chochote unachokimiliki?
- Ndiyo Mtume wa Mwenyezi Mungu ninayo.
- Una miliki nini?
- Mwenyezi Mungu ameniwezesha kumiliki ngamia, kondoo, farasi, shayiri na ngano.
- Baada ya kutaja vitu anavyomiliki Mtume (S.A.W) akamwambia mtu yule:

- Kama Mwenyezi Mungu amekupa vitu vya kumiliki basi angependa kuona kiashiria cha mali alizokupa.

Yule mtu akaona aibu kutokana na mwonekano wake usiovutia. Mtume alimsisitiza ahakikishe kwamba anonekana nadhifu. Kwa sababu hata mara moja hakutaka Mwislamu adharauliwe kwa sababu ya mavazi yake. Waislamu wanapaswa kuwa mfano wa kuigwa katika mavazi na tabia.

Kuanzia siku ile yule mtu alikuwa makini na mwonekano wake. Alijitahidi kuvalaa vizuri na kwa unadhifu.



MTU ANAYEISHI JANGWANI

*M*sume wetu (S.A.W) alikuwa hawezi kutotenda haki kwa maswahaba zake na hakushindwa kuonyesha upendo kwa mtu yeyote. Aliwajali sana watu wenyewe ulemavu, wagonjwa na wenyewe uhitaji. Muumini anayeitwa Zahir alikuwa mionganoni mwa watu aliowajali sana.

Zahir alikuwa anajisikia unyonge kwa sababu ya ulemavu katika mwili wake na alikuwa hapendi kwenda sehemu yenyewe watu wengi. Kwa sababu hiyo, alikuwa anapenda kukaa mashambani. Kwa sababu alikuwa anampenda sana Mtume (S.A.W) kuna wakati alikuwa anampelekea mazao anayoyalima kule jangwani na Mtume (S.A.W) alikuwa anampa zawadi ya vitu vinavyopatikana mjini. Mtume alikuwa anamwambia Zahir:

- Zahiri ni shamba letu na sisi ni mji wake.

Siku moja Zahir alienda tena mjini. Akaanza kumsubiri Mtume (S.A.W) karibu na soko. Mtume wa Mwenyezi Mungu alimwona kwa mbali Zahir aliyekuwa anamsubiri. Kisha akasogea taratibu kwa upande wa nyuma yake. Akamkumbatia na kumziba macho kwa mikono yake. Zahir akawa anahangaika na akaanza kupiga kelele:

- Wewe ni nani? Ondoa mikono yako!

Lakini baada ya muda akagundua kwamba aliyemziba na mikono alikuwa Mtume (S.A.W)

Alifurahi sana kwa sababu Mtume (S.A.W) alionekana mtu wa kawaida kwake. Aliacha kuhangaika na kuinama kwenye kifua cha mtume. Mtume wa Mwenyezi Mungu akaendelea na utani wake na kuanza kuongea kwa nguvu:



- Nina mtumwa ninamuza ni nani anataka kumnunua?

Watu waliomwona Mtume (S.A.W) akiwa karibu sana na Zahir walikusanyika na kuanza kuwaangalia kwa furaha. Kisha Zahir akasema kwa sauti ya huzuni:


Oooh! Mtume wa Mwenyezi Mungu! Ni nani anayetaka mtu asiye na thamani kama mimi?

Mtume wa Mwenyezi Mungu akabaini kwamba Zahir alikuwa anaumia na kumwambia:

- Hapana Zahir ninakuhakikishia kwamba wewe una thamani kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Kwa sababu hiyo sisi tunakupenda.

Yule mtu ambaye alikuwa ametokea mashambani akawa na furaha, Kuwa na thamani mbele ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake ni bora kuliko kitu kingine ulimwenguni.

Kuanzia siku hiyo, Zahir hakujisikia unyoge kutokana na ulemavu katika mwili wake. Kitu muhimu kilikuwa ukunjufu wa moyo wake. Mtu aliyemfundisha haya ni Mtume wetu (S.A.W) mtu mwema kuliko watu wote.





REJESHA KIOTA CHAKE

*M*tume wetu mpendwa (S.A.W) hakupenda mtu aumie au kuhangaika kwa kukosa haki yake. Wakati wote aliwataka maswahaba kutendeana haki na ukarimu. Yeye ni Mtume ambaye alitenda haki siyo tu kwa wanadamu bali hata kwa wanyama. Alikuwa akilinda haki za wanyama na kuwazuia wanadamu wasiwadhuru.

Kabla Uislamu haujaingia katika jamii ya Waarabu, wanyama walikuwa wakichukuliwa kama viumbi visivyo na thamani. Mathalani, ngamia ambao walikuwa wakitumiwa kama vipando wakati huo walikuwa wakifungwa



minyonyororo ya chuma maeneo ya shingoni. Wanyama hawa walikuwa wakitumika kuwabebe watu maeneo ya jangwani bila kupatiwa chakula wala maji kwa muda mrefu. Mtume wetu (S.A.W) alipiga marufuku kuwawekea ngamia minyororo katika shingo zao na aliwaamuru maswahaba kuwatendea wema wanyama hao.

Siku moja Mtume (S.A.W) alipokuwa barabarani alimwona ngamia ambaye tumbo lake lilikuwa limeingia ndani kutokana na njaa. Akamwangalia mmiliki wa ngamia na kumwambia:

- Mwogope Mwenyezi Mungu unapofuga wanyama hawa ambao hawawezi kuzungumza.

Siku nyingine Mtume (S.A.W) alikuwa akitembea na maswahaba zake, mmoja wao akamwona ndege juu ya mti. Pembeni ya ndege huyo kulikuwa na kiota kizuri ambacho ndani yake kulikuwa na mtoto wa ndege. Mama wa ndege huyo alikuwa akiimba kwa furaha karibu na mwanaye. Swahaba (r.a) akataka kumbembeleza mtoto wa ndege, akachukua kile kiota na kukibeba katika viganja vyake. Mama wa yule ndege alipoona kitendo hiki akaanza kuruka mbele ya swahaba kwa haraka. Wimbo wake wa furaha aliokuwa akiimba awali sasa ukageuka na kuwa kelele za huzuni. Hali hii ilikuwa ni kana kwamba ndege yule anataka kusema "mwache mwanangu"

Mtume (S.A.W) alipoona hali ile aliuliza:

"Ni nani anayemuumiza ndege huyu kwa kumchukua mwanaye?"

Kisha Mtume (S.A.W) akamuamuru yule Swahaba "rejesha kiota chake."

Mara moja Swahaba akarejesha kile kiota alipokitoa

Mtume (S.A.W) akasema: "Ninaapa mbele ya Mwenyezi Mungu. Hakika ye ye anawapenda waja wake kuliko vile ambavyo mama anawapenda watoto wake.

Maswahaba (S.A.W) walifurahi sana kusikia habari hizi.

Nani asiyetamani kupendwa na Mwenyezi Mungu, Mola wa ulimwengu wote?





MGENI KATIKA NYUMBA YA MTUME (S.A.W)

Kijana Abdullah ni mtoto wa ami yake Mtume aitwaye Abas. Kijana huyu nadhifu na mwenye tabia njema alikuwa anampenda sana Mtume (S.A.W). Alikuwa akienda mara kwa mara msikitini kumtembelea Mtume (S.A.W). Alikuwa akifurahi sana anaposikiliza mawaidha ya Mtume na kuswali nyuma ya Mtume (S.A.W). Abdullah alipendelea kumtembelea Mtume (S.A.W) siyo tu anapokuwa msikitini bali pia anapokuwa nyumbani kwake. Alikuwa akishangazwa na namna ambavyo Mtume wa Mwenyezi Mungu alijenga uhusiano bora na familia yake na namna ambavyo alikuwa akiishi na wake zake na watoto wake.

Mambo haya yalikuwa yakimshangaza sana Abdullah.

Mmoja wa wake za Mtume (S.A.W) alikuwa ni mama yake mdogo Abdullah (r.a). Siku moja Abdullah alikwenda kwa mama yake mdogo na kuuliza:

Mama mdogo, ninaweza kukutembelea usiku? Mama yake mdogo alimshika kichwa huku akitabasamu:

- Naam, unaweza kuja. Sisi tunapenda sana wageni. Alijibu mama yake mdogo Abdullah (r.a).

Abdullah (r.a) alikuwa akisubiria kwa hamu muda aliopanga kwenda kutembelea nyumba ya Mtume (S.A.W) ufile. Hatimaye jua likazama na muda wa miadi ukafika. Abdullah (r.a) akagonga mlango nyumbani kwa Mtume (S.A.W) kwa furaha. Mama yake mdogo akafungua mlango. Baada ya muda Mtume (S.A.W) akarejea nyumbani. Alipomwona Abdullah (r.a) akatabasamu kwa furaha. Daima aliwapenda wageni wake, iwe ni watu wazima au watoto. Alimuuliza Abdullah (r.a) kuhusu afya yake. Wote waliketi katika meza ya chakula wakala chakula cha usiku kwa furaha.


Baada ya chakula cha usiku walizungumza kwa muda mrefu. Abdullah (r.a) alifurahi sana. Mtume wetu (S.A.W) alionesa upendo wa dhati kwake, hivyo Abdullah alijiona kama mtu aliyethaminiwa sana na Mtume (S.A.W). Alitamani muda usiishe ili aendelee kuwa karibu na Mtume (S.A.W). Ukafika muda wa kwenda kulala. Abdullah (r.a) akataka kulala chumba kimoja na Mtume (S.A.W). Mtume (S.A.W) anazifahamu vyema tabia za watoto na haikumchukua muda mrefu kufahamu kile ambacho Abdullah (r.a) alikuwa akikitamani. Akamshika Abdullah mkono na kwenda naye chumbani kwake. Wakalala kitandani na kupitiwa na usingizi.

Abdullah (r.a) aliamka usiku wa manane. Hakumwona Mtume (S.A.W) kitandani. Alipoangalia huku na huko chumbani alimwona Mtume (S.A.W) akitazama juu. Wakati huohuo Mtume alikuwa akiomba aya katika Kur'an. Abdullah (r.a) alimwangalia huku akistaajabu. Kisha Mtume akaanza kuswali. Aliswali kwa muda mrefu. Baada ya kumaliza swala, aliomba dua kwa muda mrefu akiwaombea maswahaba zake na wafuasi wake. Baada ya muda mfupi ikasikika adhana ya swala la alfajir. Mtume (S.A.W) kaondoka kuelekea msikitini.

Katika usiku huu kijana Abdullah (r.a) alishuhudia kwamba Mtume wetu (S.A.W) alikuwa ni mtu mwenye sifa za pekee akiwa nyumbani kama anavyokuwa nje. Asubuhi alirejea nyumbani kwa furaha. Hataweza kuusahau usiku ule katika maisha yake yote.

KIAPO CHA MWONGO

*M*tume (S.A.W) alisisitiza umuhimu wa ukweli na alitaka maswahaba zake kuaminika katika kazi zao. Idadi ya watu waliojidai kuwa Waislamu ilianza kuongezeka kadiri Uislamu ulivyokuwa unaimarika. Baadhi ya watu walikuwa wanafiki kwa kuijunga na upande wa Waislamu na wakati mwingine kuwa upande wa maadui wa Uislamu kwa maslahi yao. Watu hawa waliitwa wanafiki.





Abdullah mtoto wa Ubai alikuwa kiongozi wa watu hawa. Tangu siku Mtume alipohamia Madina, Abdullah bin Ubai kwa sababu moyo wake ulikuwa siyo mzuri alikuwa hapendi Mtume (S.A.W) anavyowakaribisha watu katika Uislamu. Kwa hiyo ndiyo maana alishirikiana na Wayahudi ili wamdhuru Mtume (S.A.W).

Waislamu walivyopata ushindi katika vita vya Badr, Abdullah bin Ubai na marafiki zake walijisikia huzuni. Ili kuzuia Uislamu usiendee walianza kufanya mipango ya siri. Kila alipopata fursa alikuwa anaupinga Uislamu ili kuwazuia watu kuukubali. Alikuwa anaeleza vitu ambavyo havijawahi kufanyika, kumsema yeote na kuwakashifu watu wasio na hatia.

Mtume wetu (S.A.W) alikuwa anajua mambo anayoyafanya Abdullah kwa sababu kuna swahaba alifika kwa Mtume (S.A.W) mara kadhaa kulalamikia vitendo viovu vya Abdullah. Siku moja mlalamikaji alieleza kwa Mtume kuhusu Abdullah. Mtume (S.A.W) alikuwa hamhukumu mtu bila kumsikiliza kwanza. Alimwita Abdullah bin Ubai mtu huyo naye akiwepo. Pia, akamweleza malalamiko yanayomhusu kwa kutaja yale aliyoambiwa kisha Mtume wetu akamuuliza:

- Ni kweli umesema maneno haya?

Abdullah bin Ubai alikuwa haogopi kusema uwongo. Alimdanganya Mtume (S.A.W) pia. Abdullah alisema:

- Hapana, sikusema kabisa mambo hayo. Aliyekuambia haya amekudanganya. Ninaapa kwa kutumia kitabu ulichokileta wewe mimi sina hatia.

Mtume wetu (S.A.W) hakutaka kumwambia ambaye ameapa kwamba amesema ukweli kuwa ni mwongo. Hakutaka kumng'angania mtu kwamba amekosa. Aliwaonya watu kistaarabu. Kwa hiyo ile siku hakumkemea Abdullah bin Ubai. Ili kumpa Abdullah muda wa kugundua kosa lake na kumpa fursa ya kujirekebisha, Mtume aliendelea kuwa mvumilivu.

Hivyo ndivyo ilivyokuwa, Mtume wetu (S.A.W) hakuharakisha kuhukumu wala kuadhibu watu. Alikuwa anaweza hata kumsikiliza mwongo na kumpa muda wa kurekebisha makosa yake. Aliwaombea watu.

Matokeo ya maombi yake ni kwamba mambo mengi mabaya yalibadilika na kuwa mazuri na watu wengi walibaini njia sahihi.

FUNZO KWA WALE WANAOKIUKA MAKUBALIANO

*M*sume wetu mpendwa daima amekuwa mwaminifu katika kutimiza ahadi na kutekeleza makubaliano. Alipohamia Madina alisaini makubaliano ya kulinda haki za Waislamu na Wayahudi katika mji wa Madina. Kwa mujibu wa makubaliano haya hakuna upande uliopaswa kuuona upande mwengine kama adui, kila mmoja alipaswa kuishi kwa Amani. Hata hivyo, baada ya muda Wayahudi walianza kukiuka makubaliano. Walianza kuzungumza vibaya kuhusu Waislamu na kutunga mashairi ya uchochezi kuhusu Waislamu. Zaidi ya yote waliungana na maadui kuwashambulia Waislamu.

Kutokana na tabia yao ya kukiuka makubaliano, Mtume (S.A.W) aliwaita viongozi wa Wayahudi katika mkutano na kuwashawishi waingie katika Uislamu kwa kuwapa mawaidha kuhusu dini tukufu ya Uislamu. Hata hivyo, hawakuwa tayari hata kumsikiliza Mtume (S.A.W).

Kisha Mtume (S.A.W) akawataka wasaini tena makubaliano ya amani. Hata hivyo, walikataa. Licha ya maneno yote ya busara kutoka kwa Mtume (S.A.W) walitoka nje ya mkutano na kuanza kuwakashifu Waislamu kwa kusema: Hatutaki kuwa na makubaliano ya amani na Waisilamu. Hatuogopi kupigana nanyi."Wakaongeza matendo yao ya uadui katika siku zilizofuata.

Mtume wetu (S.A.W) alikuwa mvumilivu sana lakini Wayahudi walivuka mpaka. Walifanya vitendo ambavyo haviwezi kusamehewa. Kisha Mwenyezi Mungu akatoa amri, Mtume (S.A.W) akakusanya jeshi lake wakawafuata Wayahudi.



Walipowaona Waislamu Wayahudi ambao walisema "hatuogopi kupigana na ninyi" wakakimbia haraka kwenda katika ngome zao. Waislamu wakazunguka ngome zao kiasi cha kutowapa Wayahudi nafasi ya kukimbia. Baada ya mashambulio ya siku kumi na tano Waislamu wakatawala ngome zote.


Mtume wetu (S.A.W) akawakusanya mateka wote. Alitaka kwenda kufanya uamuzi kuhusu hatma yao. Baada ya muda Abdullah ibn Ubay akamwendea tena Mtume (S.A.W) na kumwomba Mtume (S.A.W) kwa kusema:

- Ewe Muhammad (S.A.W)! Tafadhalii wasamehe rafiki zangu.

Mtume (S.A.W) akageuza uso wake kutoka kwa huyu mnafiki. Kwa kuwa hakuwa akiwaamini mateka, alitaka kuchukua kila aina ya tahadhari. Hatimaye akachukua uamuzi kuhusu mateka hawa. Ikaamuliwa kwamba "Wayahudi wanapaswa kuondolewa Madina"

Siku hiyohiyo ikawa siku ya Wahayudi kuondoka Madina. Kwa furaha ya kuokoa maisha yao Wayahudi wakaondoka kwa haraka kutoka katika mji wa Madina. Abdullah ibn Ubay akapatwa na aibu ya kuondolewa kwa Wayahudi ambao aliwaita "rafiki zake"

Kisha siku za furaha zikarejea katika Mji wa Madina. Mtume (S.A.W) alikuwa mstahimilivu na mwenye kusamehe, lakini hakusita kutoa funzo kwa wasiotaka amani na kukiuka makubaliano.



MTU ALIYEFANYA MOYO WA ABUDARDA KUUKUBALI UISLAMU

*K*abla Muhammad (S.A.W) hajapewa utume watu walikuwa wanaabudu sanamu na kutegemea vitu hivi visivyo na uhai ambayo hata havikuweza kuwasaidia. Mtume wetu (S.A.W) alikuwa haabudu sanamu hata alivyokuwa mtoto na mara zote alimwamini Mwenyezi Mungu pekee. Baada ya kupewa utume aliwakaribisha watu wamuabudu Mwenyezi Mungu mmoja pekee na waache kuabudu sanamu. Lakini badala ya kukubali maneno yake watu wa Makka waliokuwa wanaabudu sanamu walimpinga vikali. Walitangaza vita dhidi ya Uislamu wakisema "Hatutakuruhusu kuzungumza vibaya kuhusu sanamu zetu".

Kuna siku Mtume wetu (S.A.W) baada ya kuhama kwenda Madina alialikwa na watu wa Madina katika mji wao. Hata hivyo, bado kulikuwa na watu wanaoabudu sanamu. Mmojawapo wa watu hao ni Abu Darda (r.a). Kijana huyu alikuwa na rafiki yake anayeitwa Abdullah (r.a). Abdullah (r.a) aliingia katika Uislamu na alikuwa anamwonea huruma rafiki yake Abu Darda kwa kuabudu sanamu. Alimwambia mara nyingi kwamba sanamu haiwezi kumsaidia wala kumdhuru na kumkaribisha katika Uislamu.

Lakini Abu Darda hakumsikiliza.

Siku moja Abdullah (r.a) alitaka kumthibitishia rafiki yake kwamba sananu haina uwezo wa kufanya chochote. Aliingia katika nyumba ya Abu Darda akiwa



hayupo nyumbani kwake. Aliona sanamu anazozibudu Abu Darda na kuzivunja vipandevipande kwa kutumia fimbo yake.

Abu Darda (r.a) aliporejea nyumbani akakuta sananu zote zimevunjika vipandevipande. Alikuwa na huzuni sana na hakuju cha kufanya. Ni nani atakayekuwa amefanya hivi? Alikuwa anataka kwenda kumtafuta mhalifu.

Kisha akasimama na kufikiri: 'Kama hizi sanamu zingekuwa na uwezo zingejitetea zenyewe, kwa hiyo hazina hata uwezo wa kujitetea zenyewe. Akaamua kuacha kuabudu sanamu kama rafiki yake Abdullah (r.a) ili aende kwa mtume kusilimu na kuwa Mwislamu.

Abu Darda (r.a) haraka sana akaenda kumtafuta rafiki yake Abdullah (r.a) Akamwambia kilichotokea. Wote kwa pamoja wakaenda kwa Mtume (S.A.W).

Mtume wa Mwenyezi Mungu akamkaribisha huyu kijana mdogo. Mtume wetu (S.A.W) aliona nuru katika macho yake kwamba imani imemwingia moyoni mwake. Siku hiyo Abu Darda (r.a) aliiingia katika Uislamu. Ombi kwa Mtume wetu mpendwa la kuingia katika Uislamu lilikubaliwa. Hakukuwa na maneno mazuri yanayotosha kueleza furaha aliyokuwa nayo Abdullah (r.a) kwa kumwona rafiki yake akiingia katika Uislamu.





KIJANA ALIYEMWOMBA MTUME AMWOMBEE

*M*tume wetu (S.A.W) alikuwa anafanya kazi zake mwenyewe. Alikuwa haombi kufanyiwa chochote na mtu yejote na aliwaambia maswahaba zake wafanye hivyo pia. Siku moja wakati anasafiri kwa ngamia, Abu Bakar (r.a) alidondosha hatamu iliyokuwa mkononi mwake. Alisimamisha ngamia haraka na kuiokota. Waliomwona wakamwambia:

- Ungetutuma sisi tukuokotee.

Abu Bakar (r.a) akasema:



- Mtume wetu (S.A.W) amenielekeza nisiwe ninaomba kufanyiwa chochote na mtu yeyote.

Mtume wetu (S.A.W) alikuwa anasambaza mali zilizopatikana vitani kwa wamiliki wake halali. Pia akawapa vitu vingi watu wa ukoo wa Bani Tujib ambao wanaishi mbali sana. Kisha aliuliza:

- Je, kuna mtu yeyote mionganini mwenu ambaye sijampa zawadi?
- Watu waliokuwa katika msafara wakasema:
- Ndiyo tumemsahau kijana mdogo aliyejikuwa anachunga wanyama.

Mtume (S.A.W) aliwaambia wamlete huyo kijana mdogo. Wakaenda kumchukua yule kijana na kumleta kwa Mtume (S.A.W). Kijana huyo mdogo akafika kwa Mtume (S.A.W) na kusema:

- Mtume wa Mwenyezi Mungu, Nilikuwa katika msafara uliokuwepo muda mfupi uliopita. Je, unaweza kunisaidia maombi yangu pia?
- Mtume (S.A.W) akamuuliza:
- Unataka nini?
- Yule kijana akasema, Ninakuomba unionbee msamaha kwa Mwenyezi Mungu na kumwomba anihurumie na kunipa utajiri wa moyoni.

Mtume wetu (S.A.W) alimwombea kijana huyu mdogo ambaye hakuomba chochote kutoka kwake na kumpa baadhi ya zawadi.

Kwa hiyo kabila la Bani Tujib wakarejea katika ardhi yao. Baada ya mwaka mmoja baadhi ya watu kutoka msafara huu walifika Makka kwa ajili ya kuhiji na kukutana na Mtume (S.A.W) Aliwauliza:

- Yule kijana mliyekuja naye mwaka jana anafanya nini sasa? Watu wa msafara ule wakamwambia Mtume (S.A.W):
- Mtume wa Mwenyezi Mungu, hatujawahi kumwona mtu anayeeleza furaha yake kwa baraka alizopewa na Mwenyezi Mungu kama huyu kijana mdogo. Hata kama watu wanetakiwa kugawana hii dunia wala asingejishughulisha.
- Mtume wetu (S.A.W) alifurahishwa na yale maneno aliyojasikia. Hii ilikuwa dalili kuwa maombi yake yamepokelewa. Akamwombea tena ili kijana yule afanikiwe. Mtume wa Mwenyezi Mungu hakuwahi kukataa maombi ya wale ambao hawafanyi kazi kwa ajili ya kupata manufaa ya duniani lakini alijitahidi kufanikisha furaha zao za ahera.

MGENI MASKINI

*M*tume wetu (S. A. W.) alikuwa anawahudumia watu maskini na kulinda haki zao. Alifanya hivyo kiasi kwamba alikuwa hawezi kumwacha mtu maskini aondoke bila kumtimizia mahitaji yake. Siku moja wakati anazungumza na maswahaba zake msikitini mtu maskini akaja kwake. Yule mtu akamwomba mtume kwa sauti ya kinyonge isiyosikika vizuri:

- Mtume wa Mwenyezi Mungu sijala kwa siku nyingi sasa. Sina uwezo wa kuvumilia tena. Una chochote unachowenza kunisiaidia?

Hali ya mtu huyu ilimfanya Mtume wetu (S.A.W) ahuzunike sana. Akatuma mtu nyumbani kwake kuwaambia walete chochote kilichopo nyumbani ili yule mtu ale. Lakini wake wa Mtume na watoto wake wakasema kwamba hakukuwa na kitu zaidi ya maji.

Kisha Mtume wetu (S.A.W) akawageukia maswahaba zake na kuwaauliza:

- Ni nani anayeweza kwenda na huyu ndugu yetu nyumbani kwake kwa usiku wa leo?
- Swahaba kutoka Ansar akasema:
- Mimi ninaweza

Kisha akamchukua yule mtu maskini na kumpeleka katika nyumba yake. Lakini mwenyeji naye alikuwa maskini. Kama ilivyokuwa kwa siku iliyopita katika hiyo nyumba siku hiyo hakukuwa na chakula cha kutosha kwa ajili ya watoto wao. Yule mwenyeji akamwambia mke wake:



Tunapaswa kumfanya mgeni wetu ajisikie huru. Wapeleke watoto wetu wakalale ili wasahau njaa zao. Kisha andaa meza. Weka chakula na zima taa. Wakati mgeni wetu anakula atafikiri kwamba na sisi tunakula pia.

Mke wake akafanya kama alivyoagizwa na mume wake. Kisha wakakaa mezani na mgeni wao. Katika chumba chenye giza wakijidai kwamba wanakula. Yule maskini akala chakula bila wasiwasi kwa sababu alikuwa hajala kwa siku nyingi. Akamaliza kula kisha akamshukuru mwenyeji wake. Kisha kaenda kulala pale alipoandaliwa na mwenyeji wake ilihali mke, mume na watoto walilala bila kula kitu.

Alipomwaga mgeni, yule mwenyeji alienda kwa Mtume (S.A.W).

Mtume (S.A.W) alipomwona alianza kusoma aya ifuatayo kama vile alikuwa anajua kilichotokea ule usiku:

"Na wakawapa (wageni wao) upendeleo dhidi yao katika yale waliyokuwa wanayahitaji ingawa wao (wenyeji) wana hali duni. Na wanaojiepusha na ubahili wa nafsi zao hao ndio wenye kufaulu kwa kweli kweli." (al-Hashr, 59; 9)

Yule swahaba maskini alifurahi sana kumuhudumia yule maskini kwenye nyumba yake. Aliona fahari katika moyo wake kumsaidia mtu ingawa na yeye alikuwa anahitaji. Kwa hiyo, aliongeza radhi za Mwenyezi Mungu na upendo kwa Mtume wetu (S.A.W). Hakuna mtu aliyejkuwa na furaha kushinda yeye siku ile.



MTUME ALIISHI MAISHA YA KAWAIDA

*M*tume wetu (S.A.W) aliishi maisha ya kawaida, hakupenda kujionyesha na ufahari na pia aliwashauri maswahaba zake kuishi maisha kama yake. Ingawa Fatma alikuwa mtoto wa mtume (S.A.W) yeye pia aliishi maisha ya kawaida, alifanya kazi zake mwenyewe. Alisaga unga wake kwa mikono yake na aliwahi kupata majeraha katika mikono na shingo kwa sababu ya kuteka maji. Baada ya kumaliza kazi zake za nyumbani na kuwashudumia watoto wake alikuwa anachoka sana.





Siku moja Ali alimwambia mke wake Fatma (r.a):

- Kwa nini usiende kwa baba yako na kumwomba mfanyakazi?

Fatma (r.a) alikubali na kwenda kwa baba yake. Akamweleza hali halisi. Mtume wetu (S.A.W) angeweza kumsaidia mtoto wake lakini alitaka mtoto wake ajifunze kukabiliana na matatizo ya maisha na siyo kuifikirisha akili yake na mambo ya dunia kwa kuishi maisha ya kifahari.

Kwa hiyo akamwambia:

- Fatma Mwogope Mwenyezi Mungu! Mwabudu! Fanya kazi za nyumbani kwako. Kufanya hivi ni bora kuliko kuwa na mfanyakazi.

Fatma (r.a) alikuwa kamwe hampingi baba yake kwa hiyo alikubali na kuondoka pale akisema:

- Ninafurahishwa na Mwenyezi Mungu na Mtume wake (S.A.W).

Siku moja Fatma (r.a) alinunua pazia jipya la rangi ya silki kwa ajili ya kuweka nyumbani kwake na kuwalisha watoto wake Hassan na Hussein (r.a) saa za rangi ya fedha. Siku hiyo Mtume (S.A.W) alienda nyumbani kwa Fatma (r.a) na alivyoona vitu vyote hivi alirudi nyumbani kwake bila kuingia ndani. Fatma alikuwa anamjua vyema baba yake kwa hiyo aligundua kosa lake. Alitoa yale mapazia mara moja na kuwavua watoto wake saa.

Hassan na Hussein (r.a) wakaenda kwa Mtume (S.A.W) wakiwa wanalia. Mtume alipoona wajukuu zake wana huzuni akawakumbatia. Kisha akaagiza aletewe zile saa. Akampa swahaba aliyekuwa karibu yake na kumwaambia:

- Ewe Thawban, zichukue hizi saa na uwape familia inayohitaji, Hassan na Hussein (r.a) ni familia yangu. Sitaki wapoteze radhi za Mwenyezi Mungu ambazo zinawasubiri huko ahera. Kisha Thawban (r.a) mnunulie mtoto wangu Fatma (r.a) mkufu wa bei nafuu na saa mbili kwa ajili ya wajukuu zangu (r.a).

Kwa maisha yake ya kawaida Mtume wetu (S.A.W) alikuwa mfano kwa familia yake na waumini wake.

Mtu ambaye anafuata ushauri wake atafaidika duniani na ahera.

USIWABAGUE WATOTO WAKO KWA SABABU YA JINSIA

*M*tume wetu (S.A.W) hakuwabagua wavulana na wasichana na aliwapenda watoto wote. Lakini, wakati huo katika jamii ya Waarabu, watu walikuwa wanawapenda watoto wa kiume zaidi kuliko wa kike. Pia, mtume wetu alikuwa hapendi ubaguzi uliokuwa unafanywa kwa wasichana. Alikuwa baba wa wasichana wanne warembo ambao aliwapenda sana, na kucheza nao, kuwabusu na kuwakumbatia. Alikuwa anawabeba mabegani mwao na kuwaonyesha mazingira ya mitaa ya Makka.

Baada ya kupokea ujumbe wa utume, alianza kuwaonya wazazi kuhusu kuwabagua watoto kwa kigezo cha jinsia. Siku zote alikuwa anawalinda wasichana na kuwafanya wawe na furaha kwa kuwapa zawadi.

Wakati akiwa amekaa msikitini na maswahaba zake wakiwa wanazungumza mvulana mdogo akaingia msikitini. Aliangalia kila sehemu na macho yake yenye shauku. Ilikuwa ni dhahiri kwamba alikuwa anamtafuta baba yake. Baada ya muda akamwona baba yake. Akamfuata haraka na kukaa katika mapaja yake. Baba yake akampakata na akambusu.

Kisha msichana mdogo akaingia msikitini. Pia alionekana anamtafuta mtu. Akawangalia watu kisha akaenda mbele taratibu. Akatabasamu alipomwona baba yake



akiwa na kaka yake. Kisha akawafuata. Alikuwa mtoto wa yule baba ambaye muda si mrefu alimkumbatia mtoto wake wa kiume. Yule baba hakujishughulisha na binti yake na akamwangalia kama vile alitaka kumuuliza ni kwa nini ameenda pale?"

Kisha akamkalisha karibu yake.

Mtume (S.A.W) aliona tukio lile na kumuonya asiwabague watoto kwa kigezo cha jinsia kwa kumwambia:

- Ni kwa nini hukuwatendea kwa usawa?

Baba yule hakuwa na jibu kwa sababu alibaini kosa lake.

Bila shaka baada ya ile siku, alimpenda mtoto wake wa kike kama anavyompenda mtoto wake wa kiume na kuwatendea kwa usawa.



MTUME ALIKUWA ANAPENDA UTANI

Mtume wetu (S.A.W) alikuwa makini, anayejali utu na msimamo lakini pia alikuwa rafiki na mkweli kwa watu wanaomzunguka. Alikuwa anapenda kufanya utani, alipenda watu wake wawe na furaha. Hii ndiyo sababu maswahaba zake hawakuogopa kwenda kwake wakiwa na shida. Walikuwa wanazungumza naye bila wasiwasi na walimweleza matatizo yao na kumwomba ushauri

Siku moja mwanamke mzee alienda kwa Mtume (S.A.W) na kumwambia:

- Eee mtume wa Mwenyezi Mungu! Je, unaweza kuniombea niingie Peponi?

Mtume wetu (S.A.W) akamtania kwa kumwambia:

- Mwanamke mzee hawezi kuingia peponi

Kisha yule mwanamke akaondoka pale akiwa analia.

Mtume (S.A.W) akawaambia maswahaba zake akiwa anatabasamu:

- Nendeni mkamwombie "Wewe ukiwa mwanamke mzee huwezi kuingia peponi." Na kisha mumfanfulie kwamba Mwenyezi Mungu anasema katika Qur'an:

**"Tumewaumba wao (wanawake)
kwa namna ya kipekee na tukawafanya
kuwa vijana kana kwamba ndio kwanza**



wanaolewa, watawapenda waume zao wakiwa na umri unaolingana." (al-Waqi 'ah, 56: 35-37) Hii ina maana kwamba katika maisha ya peponi hakuna kuzeeka na kwamba hata wale wanaojiona wazee wakiwa peponi watakuwa vijana.

Mwanamke atakayesikia maneno haya kutoka kwa Mtume (S.A.W) atafurahi sana. Si ndivyo?

Na kuna wakati mwingine siku moja, Mtume wetu (S.A.W) alijiwa na mama Ayman na kumwambia:

- Mtume wa Mwenyezi Mungu, Mume wangu anakualika nyumbani.
- Mtume wetu akamwuuliza je, Mama Ayman Mumeo ni nani? Ni yule mwenye weupe kwenye macho yake?
- Hakuna weupe katika macho ya mume wangu ee Mtume wa Mwenyezi Mungu!
- Mtume alitabasamu na kumwambia mama Ayman ambaye alikuwa amechanganyikiwa:
- Hakuna mtu ambaye hana weupe kwenye macho yake.

Vilevile kuna siku Mtume (S.A.W) alipanga safari na Aisha. Kisha Mtume (S.A.W) akamwambia swahaba wake.

- Wewe nenda kisha akamgeukia mke wake Aisha na kumwambia:
- Tushindane kukimbia na wakaanza kushindana. Aisha (r.a) akashinda.

Baada ya miaka kadhaa kupita Mtume wetu akiwa katika safari na Aisha alimwambia swahaba wake. Wewe tangulia na akamgeukia mke wake Aisha na kumwambia:

- Tushindane kukimbia.

Wakati huo Aisha (r.a) alikuwa ameongezeka uzito. Wakaanza kukimbia lakini wakati huu Mtume (S.A.W) akashinda na akamwambia mke wake huku akitabasamu.

- Ushindi wangu uwe ushindi wako Siku ya Kiama.

Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa mtu wa usawa katika utani wake kama ilivyo katika kazi zake zote. Hakupenda kumuudhi mtu hata kama anafanya utani.

MTUME ALIWAHESHIMU WAKUBWA WAKE

*M*tume wetu alikuwa anasisitiza umuhimu wa familia yake na alionyesha upendo kwa watoto wake na wake zake kila alipopata fursa. Hakuwahi kuamua peke yake kuhusu masuala ya familia na mara zote alisikiliza maoni ya watoto na wake zake. Kwa mfano aliomba maoni ya wasichana walipotaka kuolewa na aliwapa fursa ya kuchagua waume zao.

Mbali na wanafamilia wa Mtume (S.A.W) aliwaheshimu ndugu zake wa karibu na mara zote alidumisha undungu na kuwaheshimu ndugu wa baba yake na ndugu wengine wa karibu. Alikuwa anawatemebelea walipoumwa na kuwasaidia pale wanapohitaji msaada. Hakuwahi kuwa na kinyongo au kuchukizwa na vitendo vyao. Alipoutwaa mji wa Makka aliwasamehe ndugu zake waliokuwa wanaabudu miungu ambaeo walimsumbu mwanzoni wakati anatangaza Uislamu.

Mtume wetu (S.A.W) hakusahau kabisa wema aliotendewa. Kwa mfano, mara zote alimpenda na kumheshimu mwanamke aliyemnyonyesha anayetwa Halima (r.a) aliyemlea tangu akiwa mdogo. Kila alipokuwa anamwona alionyesha shukrani kwa kumwita 'Mama' na kumuuliza kuhusu afya yake.

Wakati fulani mlezi wake Halima alienda kwa Mtume (S.A.W) na kumweleza kuhusu ukame na njaa na wanyama wanaokufa katika kijiji chao kwa njaa na kiu na matatizo ya pesa.

Akati huo Mtume wetu (S.A.W) alikuwa ameshamwoa Khadija (r.a). Alimkaribisha



Halima (r.a) vizuri. Mtume pamoja na mke wake Khadija (r.a) walimpokea Halima (r.a) katika mapokezi mazuri na kumpa zawadi. Kisha akampa kondoo arobaini ili wamsaidie kupata pesa.

Halima (r.a) alifurahishwa na wema na matendo ya Mtume wetu (S.A.W), kisha akarejea kijijini kwake akimwombea Mtume (S.A.W).

Siku moja swahaba akaenda kwa Mtume (S.A.W) na kumuuliza:

- Eee, Mtume wa Mwenyezi Mungu! Unaweza kuniambia kitendo ambacho nikifanya nitaigia Peponi?

Mtume (S.A.W) alisema:

- Unapaswa kuswali kwa usahihi, kutoa zaka na kutenda mema na uwe na uhusiano mzuri na jamaa na ndugu zako. (Bukhari, Kitabu cha Tabia na Mwenendo Bora, 10)

Mtume alikuwa mfano mzuri sana kwa maswahaba zake kuhusu kuonyesha heshima, upendo na utu kwa wakubwa zake. Si ndivyo?

WEMA WA MTUME

*H*uko Madina kulikuwa na Mwanazuoni wa Kiyahudi anayeitwa Zayd, mtoto wa Sanaa (r.a). Mtu huyu alikuwa anajuliza ikiwa ni kweli kwamba Mtume (S.A.W) ni mjambe wa Mwenyezi Mungu kama ilivyokuwa inasemwa na kwamba maadili ya Mtume (S.A.W) yalikuwa ya juu kama alivyokuwa anasikia. Ili kujua alifanya jaribio na alianza kumfuatilia Mtume (S.A.W) taratibu.

Siku moja Mtume (S.A.W) alikuwa anatembea akiwa na Ali (r.a), akajitokeza mtu mbele yao na kuuliza:

- Mtume wa Mwenyezi Mungu, ukame na njaa vinakikibili kijiji chetu. Je, unaweza kutusaidia?
- Mtume (S.A.W) akamuuliza Ali (r.a):
- Je, tuna chochote kilichosalia ili tuwapatie? Ali (r.a) alisema:
- Hakuna kilichosalia tunachoweza kuwapa Mtume wa Mwenyezi Mungu.

Kisha Zayd bin Sanaa (r.a) ambaye alikuwa anawaangalia kwa mbali akawakaribia na kuwaambia anaweza kuwakopesha tende kiasi. Hata hivyo, aliweka masharti ya siku ya kulipwa tende zake. Mtume wetu (S.A.W) alikubali masharti ya Zayd. Hivyo, alikopa tende kutoka kwa Zayd na kumpa yule maskini na kumwambia apeleke hizo tende kijijini kwake na azigawe kwa wanakijiji.



Muda ukapita kidogo. Siku moja, Mtume wetu (S.A.W) alikuwa anatembea akiwa na Umar (r.a), ghafla Zayd akawasimamisha na ingawa haikuwa siku ya kulipwa akaanza kugomba kwa nguvu.

- Muhammad (S.A.W) lipa deni unalodaiwa! Mbona hujalipa deni ninalokudai? Umar (r.a) akaanza kumfuata Zayd kwa hasira na kumkaripia akisema:

- Wewe adui wa Mwenyezi Mungu! Unawezaje kuzungumza kwa ujeuri hivyo kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu?

Alitamani kumpiga.

Zayd bin Sanaa (r.a) akaondoka kwa sababu ya kumwogopa Umar (r.a) wakati Mtume wetu (S.A.W) alikuwa amenyamaza tu. Akamgeukia Umar (r.a) na kumwambia:

- Umar (r.a) ulipaswa uniambie nilipe deni langu ingawa siku ya kulilipa haijafika bado, na ulipaswa kumshauri huyu mtu kuuliza kuhusu deni lake kwa ustaarabu. Mwondoe hapa na mlipe deni lake. Mwongezee tende kidogo kwa sababu umemtishia.

Umar (r.a) akaondoka na yule mtu na kumlipa tende zaidi ya zile anazodai kama alivyoelekezwa na Mtume (S.A.W).

Kwa hiyo, Zayd (r.a) akaona namna ambavyo Mtume wetu (S.A.W) alivyojibu kwa namna ya kuonyesha ukomavu dhidi ya ukorofi na kutokuheshimiwa. Ndiyo huyu si mtu mwingine bali ni Mtume wa Mwenyezi Mungu ambaye amemsoma katika vitabu. Moyo wake ulijawa na imani na haki na aliamua kubadili dini na kuwa Mwislamu.

Uvumilivu na tabia njema ya Mtume wetu vikaonesha ubora mwingine katika Uislamu.



FURAHYA YA MSICHANA MDOGO

*S*iku moja Mtume wetu (S.A.W) alienda kununua shati dukani. Alipotoka tu kwenye hilo duka akaja mtu maskini karibu yake na kumwomba Mtume (S.A.W) kama ifuatavyo:

- Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Tafadhali nivalishe shati na Mwenyezi Mungu atakuvalisha nguo za Peponi.

Mtume wetu (S.A.W) alimwonea huruma mtu huyu aliyejewa amevaa nguo zilizochakaa. Akampa lile shati jipya alilokuwa ametoka kulinunua. Kisha akarudi dukani kujinunulia shati jingine. Alikuwa na sarafu mbili tu zilizobakia katika mfuko wake kati ya sarafu kumi alizokuwa nazo.

Alipokuwa njiani kurejea nyumbani kwake alimwona msichana mdogo. Alikuwa analia na kuangalia huku na kule. Mtume wetu (S.A.W) akamuuliza kwa nini alikuwa analia. Alisema huku analia kwa sauti ndogo:

- Tajiri wangu alinipa sarafu mbili za fedha nikanunue unga. Lakini nimezipoteza hizo pesa ndio maana ninalia.

Mtume wetu (S.A.W) alikuwa hapendi kumwona mtoto anahuzuni. Kwa hiyo akazitoa zile sarafu mbili za fedha zilizosalia na kumpa yule msichana. Akamwambia aende akanunue unga.

Hata hivyo hakuacha kulia. Mtume (S.A.W) akamuuliza:

Mtoto mzuri kwa nini bado unalia wakati nimeshakupa hela?

Mara hii mtoto akasema:

- Wakati natafuta hela nilizokuwa nimepoteza nimechelewa sana kurudi nyumbani na nitagombezwa na tajiri wangu.



Mtume wetu (S.A.W):


- Usiogope mwanangu, twende wote. Akamshika mkono na kumpeleka hadi nyumbani kwao.

Tajiri wa yule mtoto alipomwona Mtume (S.A.W) alisema:

- Karibu Mtume wa Mwenyezi Mungu! Umepata tabu kufika hapa.
- Mtume wetu (S.A.W) akasema:
- Huyu msichana mdogo alikuwa anaogopa kwamba unaweza kukasirika kwa sababu amechelewa, kwa hiyo nimemleta. Yule tajiri alifurahi kumwona Mtume wa Mwenyezi Mungu na akamwambia:
 - Mtume wa Mwenyezi Mungu, umetuheshimu kwa kuja katika nyumba yetu kwa hiyo tunamwachia awe huru. Kama atakubali kuendelea kuishi na sisi hatakuwa mtumwa tena bali binti yetu.

Maneno haya yalimfanya Mtume (S.A.W) awe na furaha. Akawaombea wanaoishi katika nyumba hiyo kwa kusema:

- Ee, Mwenyezi Mungu! Ni thamani ya kiasi gani ilikuwa katika sarafu kumi za fedha ulizoniruzuku! Umenivalisha mimi shati pamoja na yule mtu maskini na umembariki huyu msichana mdogo kuachiliwa huru.



EWE BILAL (R.A)! TOA ADHANA!

*M*tume wetu mara zote alikuwa anawalinda watu maskini waliokuwa wanamzunguka na kuwasaidia. Watu walimpenda sana. Mara kwa mara walikuwa wanamtembelea na kujifunza dini yetu.

Siku moja wakati Mtume wetu (S.A.W) alikuwa amekaa msikitini, kundi kubwa la watu lilimtembelea. Walikuwa wamevaa nguo zilizochakaa. Walikuwa wamevaa kipande cha kitambaa ambacho wamekitoboa katikati na kupidisha kichwa katikati yake. Walikuwa hawajavaa viatu na ilikuwa rahisi kubaini kwamba watu wale ni maskini.

Mtume wetu (S.A.W) alihuzuni sana alipowaona. Alienda nyumbani kwake haraka kutafuta namna ya kuwasaidia. Hata hivyo, hakukuwa na chochote nyumbani kwake cha kuwapa watu wale. Alirejea msikitini akiwa na huzuni sana lakini hakutaka watu hawa warejee kwao bila kupata chochote. Alimwita Bilal (r.a) na kumwambia:

- Ewe Bilal toa adhana.

Bilal (r.a) aliadhini kwa sauti nzuri. Waislamu waliosikia adhana walikimbia kuelekea msikitini. Msikihi ulijaa watu ndani ya muda mfupi. Mtume wa Mwenyezi Mungu akatoa mawaiidha kuhusu umuhimu wa kuwasaidia maskini katika dini yetu, akasoma aya za Qur'an na kisha akasema:

- Toa sadaka kwa maskini hata kama ni nusu ya tende. Baada ya kusikiliza mawaiidha ya Mtume (S.A.W), maswahaba zake wakakimbia nyumbani. Baada ya muda



walirudi na vitu vingi mikononi mwao kwa ajili ya kuwapa wale maskini waliokuwa msikitini. Kisha baadaye msikititi ulijaa nguo, viatu na chakula.

Mtume wetu (S.A.W) alikuwa na furaha sana kutokana na ukarimu wa maswahaba zake na akasema kuwa kila kilichotolewa kama sadaka kitatumika vizuri. Kisha akaongezea:

- Mwenyezi Mungu atawapa vitu vingine badala ya vile mlivyotoa sadaka.

Kisha vitu vilivyokusanywa vikagawanywa kwa wale maskini. Walifurahi sana kwa msaada walipewa. Waliondoka mjini kwa furaha na kumshukuru mtume (S.A.W).



PEANENI SALAMU

*M*sume wetu (S.A.W) aliweka msisitizo mkubwa kuhusu kusalimiana, hakuchukia watu na alikuwa makini kuhusu kutabasamu.

- Alikuwa anawaelekeza maswahaba zake (r.a) kuzingatia suala hili:





- Hamtaingia Peponi kama hamtaamini na hamtaamini kama hamtapendana. Na kupeana salamu ni ishara ya kupendana. Nawaambieni kitu ambacho mkikifanya kitaimarisha upendo mionganoni mwenu: Endezeeni utamaduni wa kusalimiana kwa kusema Assalam alaykum.

Mtume wetu (S.A.W) alipoenda kwenye nyumba ya mtu, kulingana na utamaduni alisimama nje ya mlango na kubisha hodi kwa kusalimia:

- Assalam alaykum.

Siku moja asubuhi alienda kwenye nyumba ya Ali (r.a) na mwanaye Fatma (r.a). Alikuwa haingii kwenye nyumba ya mtu bila kubisha hodi na kusalimia hata kama ilikuwa ni kwenye nyumba ya mwanaye. Siku hiyo alibisha hodi akiwa amesimama mlangoni:

- Assalam alaykum.

Ali (r.a) na Fatma (r.a) walalisikia salam ya Mtume, lakini walikuwa bado wamelala. Walisita kujibu salamu ya Mtume kwa sababu walihisi Mtume angewaona wao ni wavivu. Mtume akasalimia tena lakini Ali (r.a) na Fatma (r.a) hawakujibu kwa sababu waliona aibu. Kwa mujibu wa utamaduni wao mtu anayeenda kwenye nyumba ya mtu mwininge anapaswa kusalimia mara tatu na kama mlango hautafunguliwa baada ya kusalimia mara tatu anapaswa kuondoka. Ali (r.a) na Fatma (r.a) wakafungua mlango kwa kuogopa Mtume ataondoka. Wakamkaribisha kwa kusema:

- Waaleykum saalam, Mtume wa Mwenyezi Mungu!

Mtume wetu (S.A.W) amesema kwamba salamu inalainisha nyoyo na kwa sababu hiyo alikuwa anamsalimia kila mtu atakayekutana naye, awe mdogo au mkubwa. Mara nyingi watoto walipomwona walikuwa wanafurahi. Walikuwa wana mzunguka na kumsalimia kwa kumshika mkono. Mtume alikuwa anawajibu kwa upendo. Alienda nao hadi alikokuwa anaenda na hakuachilia mkono wao mpaka watakapotoa mkono wenyewe.

Waliokuwa wanasalimiwa na Mtume (S.A.W) walikuwa na furaha kiasi gani?

Na wale waliokuwa wanamsalimia walikuwa na furaha kiasi gani?

KUMSAIDIA ADUI

*U*likuwa umepita muda mrefu tangu Mtume (S.A.W) ahame kutoka Maka kwenda Madina. Waislamu walikuwa wanaishi pamoja kwa amani na utulivu. Walikuwa wanatatua matatizo yao pamoja na kufurahia kwa pamoja. Walikuwa imara kutokana na ushindi waliouopata chini ya uongozi wa Mtume (S.A.W). Madina imebadilika na kuwa mji wa Waislamu ambapo watu wanaishi kwa amani.

Hata hivyo, hali haikuwa nzuri sana Makka. Baada ya Waislamu kuhamia Madina, mji ukaanza kuwa na shida mbalimbali na machafuko kila mahali. Pia baada ya makabila ya jirani kuingia katika Uislamu upweke ukaongezeka zaidi kwa watu wa maeneo hayo.

Miongoni mwa makabila yaliyoudhihaki Uislamu ilikuwa kabilia la Hamama lililokuwa karibu na Makka. Watu wa Hamama walipoingia katika Uislamu walikuwa hawataki kufanya biashara na watu wa Makka kwa hiyo walizua kuuza ngano kwa watu wa Makka. Makka ilikuwa inapata mahitaji yake yote ya ngano kutoka kwa kabilia la Hamama. Hakukuwa na eneo lingine karibu la kununua ngano. Haukupita muda mrefu baa la njaa likaikumba Makka. Watu wa Makka wakawa wanapambana na tatizo la njaa.

Abuu Sufyan, kiongozi wa Makka akatuma ujumbe kwa kiongozi wa Hamama ili kumwomba awauzie ngano lakini hakukubali. Makka ilikuwa katika hali mbaya kwa sababu ya njaa. Mwisho kabisa wakaomba msaada kutoka kwa Mtume (S.A.W) kwa kumtumia ujumbe na kumwambia:

- Wewe ndiye kimbilio letu. Kama hutatusaidia tutakosa chakula.



Mtume wetu (S.A.W) aliwaonea huruma watu wa Makka ambao waliwaumiza Waislamu, wakajaribu kuwaua na kuwafukuza. Alifikiri kuna watoto ambao hawana hatia na wanawake wenye changamoto. Alikuwa hataki kumuacha yeyote afe kwa njaa hata kama ni adui yake.

Akatuma ujumbe kwa kiongozi wa Hamama na kumshauri awape watu wa Makka ngano.

Mtume alipoomba kitu, hakuna kiongozi yeyote aliweza kukataa ombi lake. Mifuko iliyojaa ngano ilitumwa Makka. Kwa hiyo Makka wakatumwa ngano na mkate. Watoto wakafurahi na watu wakala wakashiba tena. Kulikuwa na sherehe katika mitaa ya mji huo. Kila mmoja akamkumbuka Mtume (S.A.W) kwa kumshukuru kwa kuwakumbuka akiwa mbali.

Kupitia huruma ya Mtume wetu (S.A.W) jamii iliokolewa kwenye njaa. Mtume (S.A.W) alikuwa anaweza kumsamehe na kumsaidia adui yake kwa moyo wake uliojaa huruma na upendo.




USHINDI WA NAFSI

Makka kulikuwa na kijana mdogo anayeitwa Iqrinah. Alikuwa mtoto wa Abu Jahl na pia alikuwa adui wa Uislamu kama baba yake. Alifanya mambo yote mabaya kwa Mtume (S.A.W) na Waisalamu. Kama inavyoelezwa katika msemo usemao maji hufuata mkondo, watu walikuwa wanaumizwa na vitendo vyao. Siku ya ushindi wa Waislamu Makka ilikuwa siku mbaya sana kwa Iqrinah. Inawezekana alikuwa anaadhibiwa kwa vitendo vyake. Akaamua kukimbia kwa sababu ya hofu. Alikuwa anataka apate meli itakayompeleka Yemen na kutoroka na kwenda mbali.

Hatimaye akafika bandarini na kuingia katika meli. Meli ikang'oa nanga na kuanza kuelea kwenye Bahari ya Shamu. Iqrinah alifurahi kuona meli inaondoka na akawa anasema "meli ikifika mbali hakuna atakayeweza kuniona na nitaishi kwa amani"

Lakini baada ya muda mfupi, kukatokea dhoruba. Meli ikaanza kuyumba kuelekea kulia na kushoto utadhani imetengenezwa kwa karatasi. Meli ilikaribia kuzama. Iqrinah alikuwa hajui cha kufanya kwa sababu ya hofu. Akaanza kujuta kwa kusema:





- Ooh, Mwenyezi Mungu ninaahidi kama nikipona katika janga hili nitaenda kwa Muhammad (S.A.W) na kusilimu.

Baada ya meli kuyumba katika dhoruba kwa muda mrefu, ikasimama.

Siku moja baada ya ushindi wa Makka, Ummu Hakim (r.a) mke wa Iqrumah aliukubali Uislamu kwa kuja kwa Mtume (S.A.W). Alitamani mume wake pia aukubali Uislamu kama yeye. Akamwambia Mtume (S.A.W):

- Mtume wa Mwenyezi Mungu Iqrimah amekimbilia Yemen kwa kuogopa adhabu ya vitendo vyake vibaya. Naomba umsamehe ili arejee.

Kwa hiyo akamwombea mume wake msamaha. Mtume wa Mwenyezi Mungu akamsamehe kwa kusema:

- Alishasamehewa.

Ummu Hakim kaenda Yemen kumtafuta mume wake. Iqrimah alifurahi sana alipomwona mke wake. Ummu Hakim akamweleza kwamba amesamehewa na anaweza kurejea Makka. Iqrimah alikuwa tayari anataka kurejea nyumbani kwake na kuonana na Mtume (S.A.W). Wakarejea Makka kwa furaha.

Mtume wetu (S.A.W) alifurahi kukutana na Iqrimah:

- Karibu kijana uliyekimbia mji wa Makka

Iqrimah (r.a) alishika mkono wa Mtume ambaye hakusema neno lolote baye kwake pamoja na kwamba alimfanyia mambo mengi mabaya. Halikadhalika, akaukubali Uislamu kwa kusema: "**Ashadu an la ilaha ilallah wa ashadu anna Muhammadan Abduhu wa Rosuluh.**" Yaani ninashuhudia kwamba hapana Mola apasaye kuabudiwa ila Mwenyezi Mungu pekee na Muhammad ni mtume wake.

Mtume (S.A.W) alimhurumia na kumsamehe Iqrimah. Tangu siku ile alikumbukwa kwa matendo yake mema na akawa Mwislamu mzuri aliyeipenda dini na alitii amri za Uislamu.

MTUME (S.A.W) ALIKUWA ANASIKILIZA MALALAMIKO

*M*tume (S.A.W) akiwa na maswahaba zake alikuwa anaandaa mazungumzo na makabila ya Madina yasiyo ya Waislamu na kuwakaribisha katika Uislamu. Kabilia la Tay lilikuwa mionganini mwa makabila yasiyo ya Waislamu, kwa hiyo Mtume (S.A.W) alituma kikundi cha maswahaba katika kabilia hili ili wawakaribishe katika Uislamu. Adiy ibn Hatam, kiongozi wa hili kabilia, alikimbia aliposikia Waislamu wanakuja.

Maswahaba (r.a) walipigana na watu wa kabilia hili, wakawadhibiti na kuwapeleka mateka Madina. Dada yake Adiy bin Hatam anayeitwa Safana alikuwa mionganini mwa mateka. Mtume (S.A.W) aliwahudumia mateka vizuri na hakuruhusu mtu yeyote akiuke haki zao. Alipogundua kwamba Safana ni dada wa Adiy bin Hatam alimwachilia huru na kumwambia akamtafute kaka yake na amrudishe Madina.

Kwa furaha ya kuachiliwa huru, Safana alienda kumtafuta kaka yake. Hatimaye, alimpata na kumwambia Mtume (S.A.W) siyo mtu wa kuogopwa, akamwambia kwamba alimhudumia kila mtu vizuri hata mateka na kwamba Mtume (S.A.W) alikuwa anataka kuonana naye. Adiy bin Hatam alimsikiliza dada yake huku akiwaza ikiwa Mtume (S.A.W) ni mtu mzuri kama dada yake anavyosema. Walifika Madina na kwenda kwa Mtume (S.A.W). Mtume (S.A.W) alikuwa amekaa msikitini. Adiy bin hatam akajitambulisha kwa



Mtume (S.A.W) ambaye alifurahi sana kumwona kiongozi wa kabile la Tay. Alimkaribisha kwa uso wenyewe furaha na anataka kukaa naye nyumbani kwake.

Wakakaa chini pamoja. Ghafla mwanamke mzee akafika na kusimama mbele ya Mtume (S.A.W) na kuanza kuelezea matatizo yake, shida na mahitaji. Mtume (S.A.W) alimsikiliza yule mwanamke kwa umakini wakati anaongea na hakuonekana kuchoka kumsikiliza.

Adiy bin Hatam (r.a) alikuwa akiangalia tukio hili kwa umakini. Katika Kabilalike hakuna mtu angeweza kufika sehemu aliyopo kama alivyofanya yule mwanamke. Maskini na wanaohitaji msaada walikuwa wanashughulikiwa na wasaidizi wao tu lakini Mtume (S.A.W) alionyesha huruma na kumsaidia yule mwanamke.

Baada tu ya kufika kwenye nyumba ya Mtume (S.A.W) Mtume alitandika mto uliotengenezwa kwa nyuzinyuzi kwa ajili ya mgeni wake kukaa. Kwa sababu kulikuwa na mto mmoja tu Mtume (S.A.W) alikaa sakafuni.

Tabia hii ya unyenyekevu ilims-hangaza sana Adiy bin Hatam. Ni Mtume pekee aliyewahudumia na kuwakirimu wageni wake kwa hesima ya juu kiasi hicho.

Adiy bin Hatam (r.a) alifurahishwa na upendo na akaukubali Uislamu kwa kutamka shahada katika nyumba ya Mtume.

Ni jambo zuri sana!

Mtume wetu (S.A.W) alisababis-ha mtu mwingine kuingia katika Uislamu kutohana na tabia yake njema.



UVUMILIVU WA MTUME

*M*tume wetu mpendwa aliweka msisitizo katika elimu ya maswahaba zake wote. Elimu kwa watoto, vijana, wazee, wanaume, wanawake. Walikuwa wanajadiliana na Mtume (S.A.W) na kujifunza kutoka kwake maadili mema.

Mtume (S.A.W) alitenga siku moja kila wiki kwa ajili ya waumini wanawake. Siku hiyo waumini wanawake walikusanyika msikitini na kuzungumza na Mtume (S.A.W) na kumuuliza maswali kuhusu dini.

Siku moja wanawake walienda kwa Mtume (S.A.W). Wanawake wote walikuwa na shauku ya kumuuliza Mtume (S.A.W) maswali. Walianza kuuliza maswali mmoja mmoja. Mtume (S.A.W) aliwasikiliza kwa makini na kujaribu kutafuta suluhisho la matatizo yao. Lakini baadaye kidogo kelele zikaanza kusikika kutoka ndani. Wanawake walikuwa wanagombana.

Kisha, Umar (r.a) aliomba ruhusa ya kuingia. Wanawake waliosikia sauti ya Umar (r.a) waliacha kuzungumza na kukaa kimya kwa muda. Alipoingia hawakusema kitu.

Mtume wa Mwenyezi Mungu alimwangalia Umar (r.a) huku anacheka. Umar (r.a) akamuuliza:

- Maisha yangu nayatoa kwako Mtume wa Mwenyezi Mungu. Ninamwomba Mwenyezi Mungu akupe furaha muda wote. Mbona unatabasamu?

Mtume (S.A.W) alimjibu huku akiwa anatabasamu zaidi:



- Watu wote walionizunguka waliacha kuzungumza na kukaa kimya baada ya kusikia sauti yako. Nilipenda walichofanya. Umar (r.a) alisema:

- Ndiyo walipaswa kukuogopa. Kisha akamgeukia mwanamke na kumuuliza:

Je, unaniogopa mimi na si Mtume wa Mwenyezi Mungu?


Yule mwanamke akasema:

- Ndiyo! Wewe ni mkali na si mvumilivu kama Mtume wa Mwenyezi Mungu Mtume wetu (S.A.W) baada ya kusikia walichokisema akasema:

- Wamesema kweli Umar (r.a) Shetani akikuona barabarani atabadilisha njia yake kwa kukuogopa.

Baada ya maneno haya vicheko vikasikika msikitini.

Kutokana na uvumilivu na wema wa Mtume (S.A.W) alipendwa na kila mtu.





HOTUBA YA KUAGA

Mtume wetu mpendwa alifika Makka tarehe 9 mwaka wa Hijra na kutembelea Alka'aba akiwa na maswahaba wake. Hii ilikuwa ziara ya mwisho katika nyumba ya Allah. Kwa hiyo iliitwa "Hija ya Kuaga. Mtume wetu aliwakusanya waumini wote na kutoa hotuba iliyoitwa hotuba ya kuaga"

Baadhi ya mafundisho yalitolewa katika hotuba ya kuaga ya Mtume (S.A.W) ni haya yafuatayo:

Enyi wafuasi wangu, sikilizeni maneno yangu. Sijui kama nitapata fursa ya kuonana nanyi tena katika eneo hili miaka ijayo.

Waumini wangu. Hakika mtakutana na Mola wenu na atawauliza kuhusu matendo yenu. Kwa hiyo kuweni makini msiache kutenda matendo mema baada ya mimi kuondoka. Fikisheni ujumbe wangu kwa wale ambao hawapo hapa. Inawezekana kwa mtu aliyeko hapa kusambaza maneno haya kwa watu wengine zaidi.

Waumini wangu! Rejesheni mali mlizopewa kwa wamiliki wake. Riba za aina yoyote ni haramu.

Enyi watu! ninawashauri mlinde haki za wanawake na kumwogopa Mwenyezi Mungu kuhusu haki zao. Kumbukeni kwamba mmewachukua kama wake zenu chini ya uaminifu na kwa ruhusa ya Mwenyezi Mungu tu.

Enyi waumini! Ninawachieni mambo mawili, kama mtayaifuata hamtapotea. Mambo hayo ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu na suna za Mtume wake (S.A.W).

Mnapaswa kujua kwamba kila Mwislamu ni ndugu wa Mwislamu mwingine na kwamba Waislamu wote ni ndugu. Mola wenu ni mmoja. Ninyi nyote ni watoto wa Adam.

Enyi watu! Endapo mtaulizwa kuhusu mimi, je mtasemaje?

Waislamu wakajibu kwa pamoja:

- Umetekeleza Amri ya Allah na umetuongoza katika njia iliyonyooka. Umekamilisha lengo lako kama Mtume kwa ufanisi mkubwa.

Kisha baada ya hapo Mtume akainua kidole chake cha shahada na kukielekeza angani na kusema:

- Allah naomba uwe shahidi yangu! Allah naomba uwe shahidi yangu! Allah naomba uwe shahidi yangu!

Mtume wetu mpendwa alifikisha ujumbe wa Uislamu kwa maswahaba zake hadi siku alipofariki. Na tumerithi tabia njema kutoka kwake. Hivyo, yeye ni mfano bora wa kuigwa kwetu. Tunaomba tukutane na Mtume wetu mpendwa katika Pepo ya Mwenyezi Mungu.